# Ndoa Na Talaka
Jeffersonville, Indiana, USA
Februari 21, 1965A

1 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa muda wa maombi. Baba Mwingi wa Neema, tunakushukuru asubuhi ya leo kwa ajili ya majaliwa haya ya kuwa hapa katika ukumbi huu, tukikabili matokeo ya siku hii. Lakini hatujui siku hii inashikilia mambo gani, bali sisi twamjua Yeye Ambaye anaishikilia siku hii. Kwa hiyo tunaomba ya kwamba Yeye Ambaye anashikilia leo na kesho, na Umilele wote, atatubariki leo tunapokusanyika pamoja katika Jina Lake, tupate kujua vizuri zaidi jinsi ya kuishi kumtumikia. Hili ndilo kusudi letu kamili, Baba. Mungu, ambaye anaijua mioyo yetu, anajua hii ni kweli. Tunajikabidhi Kwako, pamoja na—na sehemu ya baadaye ya siku hii, kwa ajili ya huduma Yako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ketini.

[Ndugu Branham anazungumza na mtu fulani jukwaani — Mh.] Asanteni. Hii hapa nyingine hapa.

2 Habari za asubuhi, wasikilizaji wanaoonekana na pia wasikilizaji wasioonekana kote nchini ambapo tumeunganishwa asubuhi ya leo. Hii inanipa tunu kuu kuja hapa na kuzungumza asubuhi ya leo juu ya somo hili muhimu. Kwa wasikilizaji wanaoonekana, ni kweli kidogo linachanganya, kwa sababu mbele yangu kuna mapazia, basi sina budi kuzungumza upande wa kulia na wa kushoto. Na kwa wasikilizaji wasioonekana, nina jumba la mikutano kulia kwangu, na pia kwenye ukumbi wa michezo wa kushoto; nami niko sakafuni, huku mapazia yamefunguliwa katikati, yakifanya mkono wangu wa kuume na wa kushoto. Nasi tumejaa tele, asubuhi ya leo, kwenye jumba la mikutano, pia kwenye ukumbi wa michezo, na pia kanisa, kanisa kule chini kwenye Barabara ya Nane na ya Penn. Na katika sehemu zilimojaa watu, mfumo wa simu unaupeleka katika sehemu zile nyingine.

3 Tumekuwa na wakati mzuri sana katika Bwana, nasi tuko katika matarajio makubwa kwa ajili ya ibada hii asubuhi ya leo. Na sasa usiku wa leo ukiwa ndio wakati wa kumalizia kwa siku hizi nne za kampeni, mbona, hakika tunawakaribisha wote, wanaoweza, kuwa hapa. Tunatumaini ya kwamba Bwana atatupa kilele kikuu usiku wa leo kwa kufanya jambo lisilo la kawaida sana, hata angewaponya wagonjwa wote na kufanya mambo makuu ambayo kwa kawaida hufanya. Nasi tuko kwenye matarajio makuu jioni hii. Umma unaalikwa vizuri, kila mtu, kila kanisa la kila dhehebu. Hata haikubidi kuwa Mkristo; hakika tunawaita wenye dhambi kuingia, kuketi miongoni mwetu. Nasi tunajitahidi sana kuwafundisha njia ya Bwana, tupate kuishi.

Sasa natumaini ya kwamba wasikilizaji hawatakuwa na wasiwasi. Nami nikimtumaini Mungu kwamba sitakuwa na wasiwasi, kwani nimekuwa na usiku mgumu sana, uchovu mwingi wa akili. Kwa kuwa ninatambua ya kwamba mambo ninayosema asubuhi ya leo yatashikiliwa dhidi yangu katika Siku ya Hukumu, nami si—nisingeweza kulala, nami najua kama sisemi hayo yatawekwa dhidi yangu katika ile Siku ya Hukumu. Kwa hiyo hulifanya kuwa gumu, huwezi kulielezea.

4 Na sasa asubuhi ya leo ndilo hilo somo kuu tunalopaswa kuzungumzia juu ya *Ndoa Na Talaka*. Na sababu ya mimi kuifanya shule ya Jumapili, ili kwamba tuweze kuzungumza juu yake na kuchukua wakati wetu, badala ya kuhubiri mahubiri juu yake. Ni mafundisho kutoka kwenye Maandiko.

Nami na—nataka kusema kwamba, kama mhubiri ye yote au wahudumu, mahali po pote, iwapo kanda hii itawahi kuangukia mikononi mwao, kama tukiachilia kanda hii. Sijui kanisa litafanya nini juu ya jambo hilo. Ninamwomba Ndugu Fred aone halmashauri ya kanisa kabla hajatoa kanda hii. Na kwenu ninyi watu kote nchini, ambao mna vinasasauti, tafadhali msiruhusu kanda hiyo itoke isipokuwa msikie kutoka kwa Ndugu Sothmann kuhusu jambo hilo.

Sasa, na kama ikiachiliwa, na ye yote wa ndugu zangu wahudumu, ama Mkristo yeyote mahali popote, ambaye asingekubaliana juu ya mambo ninayosema juu ya somo hili, ni—ninatumaini ya kwamba hamtalikosoa. Kama hulielewi jinsi ninavyolifundisha, vema, una haki ya hilo, kama mhudumu, kama mchungaji. Nami naheshimu chochote unachoamini.

5 Na kuna itikadi mbili kuu juu ya jambo hili. Na kama kuna maswali mawili, hapana budi moja ya hayo yawe sahihi, ama hakuna moja la hayo lililo sahihi. Kwa hiyo tutajaribu kuliangalia Neno la Mungu, asubuhi ya leo, kulitatua hili. Kwangu mimi, kama ni swali la Biblia, hakika Biblia ina jibu lake.

Na sasa kabla tu hatujapata haya, kuanza somo hili, hasa, kabla sijaomba Neno, nataka kuwaelezea kila mmoja wenu, ya kwamba mimi … ninyi hasa Wakristo, kwamba ninataka … Na—nawatakeni mniombee asubuhi ya leo. Na wote huko kwenye wasikilizaji wasioonekana ambao wanasikiliza asubuhi ya leo, niombeeni, kwa sababu ninataka kuwa mwaminifu na mkweli.

6 Sasa tunatambua, katika kutoa matamshi haya, mtu fulani, kama ni mtu mmoja tu, atashikilia Hilo kama ilivyokuwa kati ya uhai na mauti. Kuna wengi wenu hapa watakaoondoka wakiamini. Bila shaka, wengi wenu, labda, hamtaweza. Lakini ninajua, katika huduma yangu, kuna watu wanaokuja kunisikiliza, na kusikiliza yale nitakayosema; kutoka, vema, wameketi papa hapa asubuhi ya leo, kimataifa, kutoka

wengi wa Marekani, Canada, na ng'ambo ya bahari. Nawe unaweza kuwazia mzigo linaokuwekea, kujua ya kwamba mwisho wa mtu huyo wa Milele uko mikononi mwako, maana yeye atashikilia yale unayosema. Kwa hiyo Mungu angenifanya niwajibike kwa jambo hilo, nami ninataka kuliendea hili kwa uaminifu niwezavyo.

7 Sasa na—naomba dada zetu. Nami nilibadilisha baadhi ya maneno yangu kusudi niweze kuyanena mbele yao. Billy ana mfukoni mwake, asubuhi ya leo, huko nje, baadhi ya mambo ambayo hayangeweza kusemwa mbele ya wa—wasikilizaji waliochanganyikana. Na mengine ambayo labda nitasema, hamna budi kuyaelewa. Chukua kama kutoka kwa—kutoka kwa ndugu yako, kwa kadiri nijuavyo. Ungeliketi katika afisi ya daktari na kumsikiliza yeye, ingemlazimu kutamka maneno wazi kabisa kwako. Na baadhi yenu ninyi vijana wanawake na vijana, sitaki mpate mawazo mabaya. Ninawatakeni mwuamini, na mketi tu kimya. Kumbukeni, Kweli haina budi kutamkwa Kweli.

Na, sasa, hapana shaka lakini kutakuwa na wengi wenu wasiokubaliana na yale yatakayosemwa, bali ninataka kuwathibitishia jambo hilo kwa Biblia. Na halafu ninaamini, kama tu mtakuwa na kicho na kusikiliza, basi mtakuwa na ufahamu mzuri zaidi na wazo la yale nimekuwa nikipigilia, wakati wote. Ninaamini hili litaeleza jambo hilo, nami ninatumaini ya kwamba litafafanua.

8 Sasa twaweza tukachukua muda mrefu, saa moja na nusu, au pengine zaidi, juu ya hili. Sijui itachukua muda gani.

Na sasa tena, ningetaka kusema ya kwamba, katika wakati huu, ya kwamba, nikijua ya kwamba watu wanashikilia maneno yako; wanafanya hivyo, kwa mchungaji wao. Na, bila shaka, nimekuwa mchungaji.

Nao wanashikilia maneno ya mchungaji, kama tu ilivyokuwa kati ya mauti na uzima. Wanashikilia maneno ya kuhani wao, kama tu kwamba ilikuwa ni mauti na uzima. Na bila shaka, mchungaji, labda pamoja na yote anayojua jinsi ya kufanya, yeye anawafundisha watu wake kama vile tu alivyofundishwa kwenye seminari; hapana shaka ila ni kuhani, pia, katika dini mbalimbali ambazo zina makasisi. Bila shaka, mchungaji kweli ni kuhani; ni mwombezi. Kwa hiyo, kama kasisi, katika yote anayofundishwa katika shule yake, katika seminari na nyumba za watawa, mtu aliye na uaminifu mwingi sana anasema yale hasa anayofundishwa.

Vema, basi, sina ujuzi wo wote wa seminari wala ujuzi wa utawa, wala sina kitu dhidi yake hata kidogo, bali nina maisha ya kipekee sana.

9 Niliitwa nilipokuwa mvulana mdogo tu. Na katika hii niliona ishara inayoonekana, inayosikika, Nguzo ya —ya Moto ikining'inia kwenye kichaka, akiwa na umri wa miaka saba, papa hapa kwenye Utica Pike. Baba yangu alikuwa akifanya kazi kwa Bw. O. H. Wathen ambaye alikufa hivi majuzi tu. Nawe umekisoma kitabu hicho, unajua hadithi hiyo. Na tangu wakati huo … Kule chini mtoni basi Hiyo ikatokea waziwazi mbele ya watu. Na sasa Hiyo imepigwa picha mara nyingi, nayo inaning'inia huko Washington, D.C., kama haki ya uchapishaji, katika Ukumbi wa Sanaa za Kidini, kama Kiumbe pekee cha kimbinguni ambacho kiliwahi kuthibitishwa kisayansi kwamba kimepigwa picha; Nguzo ya Moto ile ile, katika sura ile ile hasa na kila namna, ambayo iliwapandisha Israeli kutoka Misri. Ninaamini ni Yesu Kristo katika umbo la Roho, katika Uwana wa Mungu.

Kwa kuwa Yeye aliitwa "Mwana wa Adamu" wakati alipokuja kwanza, sasa anaitwa "Mwana wa Mungu," katika ule Utawala wa Miaka Elfu Yeye atakuwa "Mwana wa Daudi." Yeye alikuja Mwana wa Adamu, Nabii, kama ilivyonenwa habari Zake; sasa Yeye ni Mwana wa Mungu, katika mambo ya kimbinguni; katika ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu utakaokuja, Yeye atakuwa Mwana wa Daudi, akiketi kwenye kiti cha enzi cha Daudi. Kama wasomaji wote wa Biblia wanavyojua kwamba hiyo ni ahadi ya Kiungu aliyoahidi Mungu, akamwahidi Daudi, Yeye angemwinua Mwanawe kuketi kwenye kiti chake cha enzi.

10 Na sasa katika huduma isiyo ya kawaida, ya kipekee, nimeitwa kila kitu kutoka "Mungu" hadi "ibilisi." Na hivyo ndivyo ilivyo daima.

Hivyo ndivyo askofu mkuu wa kanisa Katoliki alivyoniambia hivi majuzi usiku kule, majadiliano yalikuwa, ya kwamba alisema, "Ndugu Branham, Yohana Mbatizaji alijitambulisha dhahiri katika Maandiko, kama alivyosema nabii Isaya." Yeye alisema, "Huduma yako imetambulishwa dhahiri katika Kanisa." Yeye alisema, "Walutheri wako katika Biblia." Yeye alisema, "Walutheri walimjua Luther. Wa Wesley wanamjua Wesley. Lakini vipi kuhusu Wapentekoste?" Kasema, "Wanazurura. Hawajui waende wapi."

Nami nikasema, "Bwana, ninathamini jambo hilo."

Na ilikuwa wakati huo Roho aliposhuka juu ya bibi huyo, hajawahi kuniona mimi, mke wake … na kunena na kutambua mambo yale yale.

Sasa, kuwa mwaminifu, kabla ya Ujumbe huu ninaozungumza asubuhi ya leo, sijui. Nilimwambia,

nikasema, "Bwana, nisingeweza kusema hivyo. Hilo ni jambo kubwa sana la kusema. Linaonekana kama lenyewe."

Jambo moja nijualo, ya kwamba kuna jambo fulani limetukia, dhahiri. Mambo haya yote, tu, yamethibitishwa kisayansi, na yanathibitishwa kote na kote ulimwenguni, haiwezi kuwa ni hadithi tu. Ni Kweli. Ni kitu gani? Hebu niseme, kwa maungamo, kabla sijawazungumzia asubuhi ya leo, sijui. Nami nisingethubutu kuchukua hatua yoyote mpaka nitakaposikia kutoka Kwake ambaye amenena nami huko nyuma na kuniambia mambo haya.

11 Kumbuka, Bwana wetu Yesu Kristo kamwe hakujitambulisha Mwenyewe kama Mwana wa Mungu. Yeye alisema, "Ulisema nilikuwa; kwa sababu hii nilizaliwa," na kadhalika, bali Yeye hakujitambulisha Mwenyewe.

Na, sasa, hiyo ilikuwa ndiyo Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli, ilikuwa ni Bwana Yesu Kristo katika umbo la Roho, (mnaamini hilo?), Ile Logos iliyotoka kwa Mungu. [Kusanyiko lilisema, "Amina." — Mh.]

Na halafu wakati alipokuwa duniani, Yeye alisema, "Nilitoka kwa Mungu, Nami ninaenda kwa Mungu." Sote tunajua jambo hilo.

Na baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka. Sauli wa Tarso alikuwa akienda zake Dameski, kuwatesa Wa—Wakristo, kwa sababu walikuwa wakifundisha mambo kinyume na yale waliyofundishwa. Naye alikuwa shujaa mkuu; chini ya Gamalieli, mmoja wa waalimu mashuhuri wa siku hizo, katika shule yao, nyumba yao ya watawa; na mtu mashuhuri, na afisa wa kanisa. Na hapo ndipo Nuru kuu, ile Nguzo ya Moto tena, ikamwangusha chini, mchana. Na Sauti ikasema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?"

12 Sasa kama ukiangalia wakati Paulo, Sauli, alipoinuka, alisema, "Bwana, Wewe ni Nani?" Sasa, mvulana huyo, akiwa Myahudi, bila shaka asingeita kitu cho chote, isipokuwa kingekuwa ni kitu fulani cha kumwakilisha Mungu, asingeweza kukiita "Bwana." Kwa hiyo, ilikuwa ni Nguzo ile ile ya Moto.

Kama vile Yesu alivyosema, "Ninaenda kwa Mungu. Nilitoka kwa Mungu, na ninarudi kwa Mungu."

Huyo hapo, amerudi katika umbo la Nguzo ya Moto tena; Yeye alisema, "Mimi ni Yesu Unayemtesa; na ni vigumu kwako kuupiga mateke mchokoo."

Nasi tunatambua ya kwamba wakati Mtume Petro, ambaye alipewa funguo za kulijenga Kanisa, tunaona ya kwamba alikuwa gerezani, na Nguzo hii hii ya Moto ilipitia kwenye fito za chuma, ikafungua milango ya gereza, na kumchukua Petro kutoka nje, kisiri, bila hata kumsumbua mlinzi. Kwangu mimi, Ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

Na ndipo daima utajua cho chote kwa asili yake. Kila kitu kinajulikana kwa asili yake, tunda kinalozaa. Nami ninawaomba mwangalie aina ya tunda kinalozaa, Nuru hii ambayo ni Mungu, kwa sababu daima hurudi kwenye Neno la Mungu, na kuthibitisha Neno la Mungu, kuhubiri Neno la Mungu, na Mungu huthibitisha Neno hilo kimwili mbele yako. Hapana budi kuwe na kitu fulani nyuma Yake.

13 Watu wameniita nabii. Mimi sijiiti nabii, kwa sababu nisingethubutu kusema hivyo, bali nina … Aisee, ninaweza kusema jambo hili, ya kwamba Bwana ameniruhusu nione mambo mbele, niwaambie mambo ambayo yametukia, yatakayotukia, yanayotukia, na hakuna hata wakati mmoja yamewahi kushindwa, katika makumi ya maelfu ya nyakati. Kila kitu alichosema kingetukia, kilitukia. Sote tunajua jambo hilo. Kama yupo mtu kwenye kusanyiko hili linaloonekana asubuhi hii, au mahali po pote, anayeweza kusema haikutukia wakati fulani, uko huru kusimama na kusema hivyo. Lakini kama kila mtu anajua ya kwamba kila wakati, kwa maelfu ya nyakati, imekuwa ni kweli kabisa, sema, "amina." [Kusanyiko linasema, "Amina!" — Mh.] Mnaona? Kwa hiyo hilo lingekuwa ni jambo lile lile kote ulimwenguni.

Jambo fulani liko karibu kutukia. Mungu kamwe hatumi mambo haya bila ya kuwa na kusudi nyuma yake.

14 Nilikuwa nikiwazia tu hapa. Niliweka hapa, moja ya maandishi yangu. Kwamba ninavaa asubuhi ya leo, seti ya viungo vya sijafu … Na wengi wenu mmesikia juu ya staa huyu wa sinema, Jane Russell, na mama yake ni Mpentekoste; na Danny Henry ni binamu yake, binamu yake wa kwanza, mtoto wa dada ya mama yake. Alikuwa Mbatisti. Alikuwa amesimama mkutanoni, mkutano wa Wafanyabiashara huko Los Angeles, California, miaka miwili iliyopita.

Nami nilikuwa tu nimemaliza kuzungumza ma—maneno makubwa mno na yenye nguvu, hata mwangalizi, mmoja wa waangalizi wakuu wa Assemblies of God, alishuka akaja jukwaani kutoka kwenye roshani ambako alikuwa ameketi, naye akasema, "Siamini kwamba Ndugu Branham alimaanisha jambo hilo."

Nikasema, "Sina budi kumaanisha jambo hilo, bwana. Ni BWANA ASEMA HIVI." Na, basi, ilikuwa ni kuhusu kanisa katika wakati huu.

15 Na yapata wakati huo, huyu kijana mwanamume ambaye mfanyabiashara… Ndugu yake amekwisha … alikuwa pale akipiga picha za televisheni asubuhi hiyo, ndugu yake mwingine ni—ni msimamizi wa barabara wa jimbo la California. Ndipo Danny Henry akaja mbele baada ya mkutano kufungwa, jukwaani, namna *hii*, ambapo watu wote walikuwa wameketi, akashuka kuja kunikumbatia. Naye akasema maneno haya, "Ndugu Branham, natumaini hili halisikiki la kukufuru, lakini," kasema, "hilo lingeweza kufanywa sura ya 23 ya Ufunuo." Ambapo, kuna sura ishirini na mbili tu katika Ufunuo. Akasema, "Natumaini hili halisikiki la kukufuru." Hakuwa na zaidi ia kulisema … Sasa, mvulana huyo alikuwa Mbatisti, wala hakujua lolote juu ya mambo ya kimbinguni. Akiwa amenikumbatia, alianza kuzungumza katika lugha isiyojulikana.

Na wakati alipomaliza kuzungumza katika lugha isiyojulikana, kulikuwa na m—mzito, mwanamke mweusi ameketi moja kwa moja mbele yangu, aliinuka, kasema, "Hilo halihitaji tafsiri yo yote." Akasema, "Ninatoka Shreveport, Louisiana, ama, Baton Rouge, Louisiana." Kasema, "Hicho ni Kifaransa dhahiri."

Victor Le Doux, ambaye alikuwa Mfaransa, pia ameketi pale, alisema, "Hakika, mimi ni Mfaransa, na hucho kilikuwa ni Kifaransa kabisa."

Nikasema, "Ngoja kidogo. *Wewe* andika yale aliyosema, nawe uandike aliyosema, kabla hujasema lolote. Andika unayosema, na tuone maandishi yako." Na kwa hiyo mmoja akaandika, na huyo mwingine akaandika, ilikuwa hata vituo vilikuwa ni sawa.

Na ndipo yapata wakati huo, wakati walipoleta maandishi hayo, mvulana mwenye sura nzuri, mwenye nywele za shaba alikuja akitembea kutoka nyuma. Ambapo, hapakuwa na nafasi ya kutosha kwake kuketi; alikuwa amesimama huko nyuma. Yeye alikuja akitembea, kasema, "Hebu kidogo, ningetaka kutoa maandishi, pia." Akasema, "Mimi ni mfasiri wa Kifaransa wa Umoja wa Mataifa, Umoja wa Mataifa." Akasema, "Ningetaka kuacha maandishi yangu."

16 Na, hapa, maandishi yote matatu yanafanana kabisa, ya Kifaransa. Na hivi ndivyo inavyosoma. Haya ni maandishi halisi yaliyoandikwa, maandishi yaliyoandikwa papo hapo. Haya ni maandishi ya Danny, mwenyewe, aliyobeba mfukoni mwake. Bila shaka, iliingia katika Wafanyi Biashara Wakristo, na kadhalika.

> *Kwa sababu umechagua njia nyembamba, njia iliyo ngumu zaidi; umetembea katika chaguo lako mwenyewe.*
>
> *Wewe umechukua uamuzi sahihi na halisi, na ni Njia Yangu.*
>
> *Kwa sababu ya uamuzi huu muhimu sana, sehemu kubwa sana ya Mbinguni itakungojea.*
>
> *Ni uamuzi ulioje wewe umechukua!*
>
> *Hili lenyewe ndilo litakalotoa na kutimiliza ule ushindi mkuu sana katika upendano wa Kiungu.*

Sasa, mtu huyo aliandika jina lake hapa. "Kauli hiyo hapo juu ilifasiriwa na … ya Danny Henry kutabiri juu ya Ndugu Branham, iliyotolewa na mashahidi watatu katika mkahawa huko Los Angeles, California."

17 Sasa, kijana huyu huyu aliyetoa unabii huu, bila kujua yale aliyokuwa akisema, alikuwa Yerusalemu yapata mwezi mmoja uliopita. Alikuwa na majaliwa ya kutoka na—na kulala kaburini ambapo Yesu alikufa na kuzikwa. Basi wakati alipokuwa amelala pale, alisema nilikuja mawazoni mwake kwa nguvu sana naye akaanza kulia. Kasema, "Jinsi ambavyo imekuwa vigumu mno kwa Ndugu Branham kusimama dhidi ya ulimwengu na mambo haya, na makanisa yote!"

Kama ilivyo—ilivyonenwa wakati mmoja kuhusu mtu mmoja, kuhusu sehemu ya Billy Graham, kasema, "Tunaweza kumwona Billy Graham, sababu makanisa yote yameungana pamoja kwa ajili yake. Tunamwona Oral Roberts, Wapentekoste. Lakini tunawezaje kuwa na cho chote, wakati ni kinyume cha yale watu wamefundishwa?" Ni Mungu.

Na, Danny, analofanya kwa kujifurahisha, hutengeneza mawe madogo. Alitoka akaenda mahali Msalaba ulipokuwa umewekwa chini, ambapo walisema Msalaba uliketi kwenye mwamba. Hakuna mtu aliyekuwa karibu naye, kwa hiyo akavunja kipande kidogo cha mwamba na kukiweka mfukoni mwake kama kumbukumbu, akaja nyumbani na kunitengenezea jozi ya viungo vya sijafu. Na, ajabu ni kwamba, alipozitengeneza, zilionekana kuwa zimetiwa damu. Na moja kwa moja katika kila moja yake, katika mfululizo, mnapita kinjia chembamba, kilichonyoka moja kwa moja ndani ya zote mbili. Sasa hiyo huenda ikawa ni … Unaona, mtu mwingine huenda asilione hilo, bali kwangu mimi ni kuidhinishwa kwa yale mambo ninayoamini. Ninaamini ya kwamba kila kitu kina maana yake.

18 Na sasa, katika wakati huu, cho chote Bwana alicho … Kama hili si jambo lile ambalo Yeye alitabiri, la Malaki 4 na pia la Luka 17, na Maandiko mengine mengi ambayo yanapaswa kutimia katika siku hizi za mwisho, hebu niseme hivi katika kumalizia, limeweka msingi kwa mtu huyo wakati atakapokuja. Kwa hiyo ninashukuru sana kwamba Mungu Mwenyezi, kama itakuwa hivyo, ameniruhusu nifanye jambo fulani dogo, katika hali yangu ya kutokuwa na elimu, kuonyesha kuthamini kwangu upendo Wake kwangu,

upendo wangu Kwake, na upendo wetu kwa watu.

Kwa hiyo, kwa unyofu, ninakaribia somo hili la *Ndoa Na Talaka*. Mungu na aturehemu sisi sote.

Na sasa sikilizeni kwa makini. Na, enyi akina dada, msisimame na kutoka; kaeni kimya kwa muda kidogo tu. Ndugu, fanyeni vivyo hivyo. Msizime redio zenu nje huko, mambo yanayowajia kwa njia hii ya simu. Usifanye hivyo. Kaeni tu kimya kwa dakika chache, mpaka itakapokwisha. Sikilizeni kwa makini. Kama hukubaliani, andika Maandiko ninayotumia, halafu uyasome kwa maombi kabla hujafanya uamuzi wako.

Mungu, tusaidie tunapojaribu kuliendea somo hili.

19 Sasa, huenda likawa refu kidogo. Sitaki muwe na haraka yo yote. Na chukueni tu wakati wenu, sisi sote, na tujifunze Neno la Mungu, kweli na kikamilifu, tunavyojua jinsi ya kulisoma.

Hebu tuanze na Mathayo Mtakatifu, mlango wa 19. Na kuanzia, nafikiri, kwa kifungu cha 8 cha mlango wa 19, ninataka kuanza. Huenda nikaanza pia na ya 1, na kusoma hadi kifungu cha 8 cha mlango wa 19.

Sasa, kumbukeni, mambo haya ninayosema hayana budi kutoka katika Neno la Mungu. Hayawezi kuwa ni maoni yangu mwenyewe, maana maoni yangu ni kama tu ya mtu mwingine yeyote. Lakini hayana budi kuwa katika mwendeleo na Neno la Mungu. Kumbuka, Mungu huweka kila kitu katika mwendeleo. Yeye habadiliki kamwe. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Unaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Yeye ni yeye yule.

Sasa nitasoma kutoka mlango wa 19.

> *Ikawa Yesu alipomaliza maneno hayo, akatoka Galilaya akafika mipaka ya Uyahudi, ng'ambo ya Yordani.*
>
> *Makutano mengi wakamfuata, akawaponya huko ...*
>
> *Basi Mafarisayo wakamwendea, wakamjaribu, ...*

Ninasimama hapo ili uweze kupata msisitizo juu ya ni nani aliyekuwa akimjaribu.

> *…wakimwambia, Je! Ni halali mtu kumwacha mkewe kwa kila sababu?*
>
> *Akajibu, akawaambia, Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke,*
>
> *Akasema, Kwa sababu hiyo, mtu atamwacha babaye ... mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawili watakuwa mwili mmoja?*
>
> *Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe.*
>
> *Wakamwambia, Jinsi gani basi Musa aliamuru kumpa hati ya talaka, na ... kumwacha?*
>
> *Akawaambia, Musa, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu, aliwapa ruhusa kuwaacha wake zenu; lakini tangu mwanzo haikuwa hivi.*

Sasa, Mungu, tusaidie.

20 Andiko hili, swali hili, lilimkabili Yesu mwanzoni kabisa mwa huduma Yake. Nalo lilimkabili Musa mwanzoni kabisa mwa huduma yake. Ni swali muhimu sana mioyoni mwa waaminio. Mwenye dhambi hajali. Lakini ni kwa ajili ya waamini, kwa sababu mwamini anajaribu kutenda yote ambayo anajua jinsi ya kutenda kuishi sawa mbele za Mungu. Kwa hiyo, swali lolote linakuja juu ya dini, ndipo kesi ya *Ndoa na Talaka* inakuja, (kwa nini?) kwa sababu ni chanzo cha dhambi ya asili. Hapo ndipo dhambi ilipoanzia. Na hiyo ndiyo sababu linaletwa kila wakati, kwa sababu ni mwanzo kabisa wa dhambi.

Sasa sitakuwa na wakati wa kuelezea mambo haya yote, bali nitafurahi kujibu barua yenu ama cho chote niwezacho. Ama, tuna vitabu vilivyoandikwa juu yake, na maswali mengi, na hata kato za magazeti na kadhalika hapa, kuthibitisha jambo hili, tunajua kwamba ilikuwa Hawa (Tofaa ambalo alidhaniwa alikula, ambapo hata si Kimaandiko, sasa wanadai ilikuwa embe dodo; haikuwa mojawapo ya hayo.), Alizini, hilo lilimleta mtoto wa kwanza, ambaye alikuwa Kaini, mwana wa Shetani, kwani ndani yake mlikaa uovu. Haukuja kwa Habili. Haukupitia kwa Habili. Mwana wa Shetani alikuwa Kaini.

21 Ninajua swali lako sasa, "Hawa alisema, 'Nimepata mtoto mwanaume kutoka kwa Bwana.'" Hiyo ni kweli kabisa.

Ungeweza kumchukua mwanamke mchafu kuliko wote mjini, mtu mbaya sana; kama wangekuwa na

mtoto, itabidi atoke kwa Bwana, kwa sababu Mungu ana sheria zilizowekwa pamoja. Na sheria hizi, kama jua kuchomoza; ukiweka gugu katika shamba zuri, litaota. Na halina budi kuota, kwa sababu ni sheria ya Mungu. Wakati mbegu inapopandwa, haina budi kuota. Na hakuna kitu kinachoweza kuotesha uhai ila Mungu, kwa sababu unafanya kazi chini ya sheria Zake. Kwa hiyo wakati uzao mwovu ulipopandwa katika tumbo la uzazi la—la Hawa, ilibidi uoteshe, kwa sababu ni sheria ya Mungu ya kuzalisha. Wala haingeweza kufanya kitu kingine ila kuuleta, na ilibidi utoke kwa Mungu.

Hiyo ndiyo sababu watu husema, "Watoto wachanga," wakati mwingine, "ambao hawajazaliwa na wazazi Wakristo, wamepotea."

Damu ya Yesu Kristo hufanya upatanisho kwa ajili ya yule mtoto, sijali amezaliwaje na alizaliwa katika uovu jinsi gani. Yeye ni Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Mtoto huyo mdogo hawezi kutubu, kwa sababu hana kitu cha kutubia, na hiyo ilikuwa ni dhambi ya ulimwengu iliyoondolewa kwa Damu ya Kristo. Watoto wachanga wanaenda Mbinguni.

22 Ni dhambi ya asili, na hiyo ndiyo sababu ina—inahojiwa. Wakati tukio lolote kuu linapotoka kwa Mungu, kuhusu jambo la kwanza: "Vipi kuhusu ndoa na talaka?" Sasa, kama ilivyowahi kuwa, bado ni swali miongoni mwa watu. Kama ilivyokuwa katika nyakati za Yesu, kama ilivyokuwa katika nyakati za Musa, daima imekuwa, na ni mpaka leo hii, swali miongoni mwa watu, kwa sababu watu wanataka kujua Kweli ni nini.

Lakini palipo na swali, lazima kuwe na jibu pia. Na sasa kwa kuwa ni jibu, kama nilivyosema hapo awali, juma hili, hapana budi kuwe na jibu sahihi. Na kama tukipata jibu la jambo lo lote, na si—si sawa, basi tunajua ya kwamba lilikuwa ni kosa. Lakini kuna, bado ungeuliza mpaka swali la kweli litakapojibiwa, kama unataka kujua Kweli. Na kwa kuwa hili ni swali la Biblia, linapaswa kuwepo jibu la Biblia.

Na kama nilivyosema, kama nilitaka kwenda mashariki asubuhi hii; na kwa yote ambayo nimejua hili, ilinibidi kutafuta kitu fulani shambani, na kilikuwa moja kwa moja mashariki, nami nilikwenda mashariki. Mtu fulani alisema, "Ndugu Branham, *hii* ni mashariki." Ni mashariki, kwa uwezekano, bali ni kaskazini mashariki. Ningepita kitu kile kile nilichokuwa nikitafuta; Ningerudi, nikijua nilikosea. Halafu basi kama mtu fulani alisema, "Ndugu Branham, nenda *huku*, upande wako wa kulia." Sasa, hiyo ni uwezekano wa mashariki, pia, lakini ni kusini mashariki. Ningepoteza kitu nilichokuwa nikitafuta, kwa sababu nilivuka mipaka ya njia kamilifu na ya moja kwa moja.

23 Sasa, kama hivyo ndivyo ilivyo, tuna mawazo mawili juu ya *Ndoa na Talaka*. Na hiyo ni kusema, mmoja wao anasema, ya kwamba, "Mtu anaweza kuoa mara moja tu, isipokuwa mkewe amekufa." Na hilo ni moja ya hayo maswali, lakini, ukiifuata hiyo, utakosa kiasi. Na halafu nyingine husema, "Loo, kama mke au mume, mmoja wao, amezini, mmoja wao anaweza kuachwa na afunge ndoa tena." Unajikuta umekosa kiasi kwa jambo hilo.

Kwa hiyo, mnaona, si kusini mashariki wala kaskazini mashariki; tunataka moja kwa moja mashariki. Ungekosa Maandiko unapoenda *huku*, unakosa Maandiko unapoenda upande *ule*. Tunataka kujua mahali Maandiko yanapokutana na Maandiko, na kujua Ukweli wake ni nini. Kila mmoja anachukua njia tofauti, na anashindwa kuleta jibu sahihi, lakini bado lazima kuwe na jibu.

24 Ni kama tu, leo, kuna itikadi mbili maarufu za mafundisho katika kanisa; moja yao ni Ukalvini, nyingine ni Uamin-…Uaminia. Mmoja wao ni mshika sheria, huyo mwingine ni neema. Nasi tunakuja kuona ya kwamba watu wanaoamini katika neema, Wakalvini, wanasema, "Mungu atukuzwe, hainidhuru kuvuta sigara. Hainidhuru kunywa pombe. Ninaweza kufanya mambo haya, nina usalama wa Milele." Halafu tunaona ule upande mwingine, wa mshika sheria, kasema, "Loo, ningetaka kumkaripia kwelikweli, ningetaka ajue ninavyosikia, lakini, mimi ni Mkristo, yanipasa ninyamaze." Mnaona, unajikuta katika barabara mbili tofauti, wala hakuna moja ya hizo zilizo sahihi. Sasa, hilo ni vigumu kusema jambo hilo, bali ni kweli.

Tunajikuta katika barabara mbili mbalimbali; moja iendayo upande mmoja, nyingine upande mwingine. Sasa hebu tuone Kweli ni nini.

25 Sasa sikiliza, uone kama jambo hili linasikika la busara kwako. Kwa mfano, kama nikiwa tayari kwenda nchi za ng'ambo. Nami nitaichukua familia yangu mwenyewe. Nitamwita mke wangu, nami nitasema, "Tunaenda- … Ninaenda ng'ambo, mpenzi." Sasa hapa kuna upande wa washika sheria, "Sasa, mke wangu, nitakuwekea sheria! Kama ukibembana na mwanamume yeyote wakati nikiwa nimeondoka, nitakaporudi wewe ni mwanamke aliyeachwa. Nami sitaki ukonyezane macho, sitaki ubembane! Mnaelewa hilo? Mimi ni mume wako! Kama ukifanya hivyo, nitakuacha nitakaporudi."

Ndipo atanijia na kunishika tai, na kusema, "Bwana wangu mwema, nataka kukuambia jambo fulani, unaona, unaona, kwamba kama ukimkonyezea macho mwanamke ye yote, au kutembea na mwanamke ye yote, au kumbemba mwanamke ye yote, utakuwa mwanamume aliyetalikiwa utakaporudi." Sasa, hiyo haingekuwa nyumba yenye furaha? Hao ni washika sheria. Vema.

Sasa, upande mwingine ni kwamba, kama nikienda nchi za ng'ambo na nikifanya kosa … Nenda kule na useme, "Sasa, angalia, nitamwacha mwanamke *huyu*. Loo, ni sawa kwa mke wangu, yeye hajali." Mke wangu anasema, "Nitatoka na mwanamume *huyu*. Ni sawa kwa Bill, yeye hajali." Kama sijali, basi nina kasoro; Simpendi mwanamke huyo vizuri. Na kama yeye hajali, ana kasoro. Yeye ni mke wangu; Sitaki mwanaume mwingine amchezee. Yeye ni mke *wangu*.

26 Sasa, njia sahihi yake, ni kwamba, kuna wote wawili wana ukweli, bali si Kweli halisi.

Sasa ninapoenda ng'ambo, kulisahihisha, familia yangu ndogo hukusanyika, nasi tunaomba pamoja. Nami ninawakabidhi kwa Mungu, nao wananikabidhi kwa Mungu. Na tunapofanya hivyo, tunaenda ng'ambo … Ninaenda ng'ambo. Sasa, ninajua ananipenda; Nina imani naye. Nami ninampenda; yeye ananiamini. Mradi tu ninampenda namna hiyo, yeye hana wasiwasi wowote kuhusu mimi kumtoa mwanamke mwingine yeyote. Mradi tu ananipenda vizuri, mbona, hakuna haja ya mimi kuwazia juu ya mwanamume mwingine yeyote kwenda pamoja naye, kwa sababu yeye ni mke wangu nami ninamwamini.

Ninaamini, kama kweli ningefanya jambo fulani baya, nifanye kosa na kwenda nje na mwanamke fulani, na kurudi tena na kama ningekiri, kumwambia, "Meda, sikukusudia kufanya hivyo. "Meda, sikutaka kufanya hivyo. Nilinaswa tu na mtego; mwanamke huyu alinikimbilia tu na—na kunikamata mkono, naye akaanza *jambo fulani*," ninaamini angeelewa. Ninaamini angenisamehe kwa jambo hilo. Lakini nisingelilitenda, hata iweje, kwa sababu ninampenda. Ingawa angenisamehe, singefanya hivyo. Nisingemwuumiza, bila sababu. Ingawa ninajua atanisamehe jambo hilo, sitaki kumdhuru.

27 Na hivyo ndivyo ilivyo kwa Mungu. Iwapo mimi…kama upendo wa *Fileo*, ambao ni upendo wa kibinadamu, upendo wa ushirika, unaweza kumfanya mti ajisikie hivyo kwa mkewe, na upendo wa *Agape* je, neno la Kiyunani linalomaanisha "Upendo wa Mungu," hilo lingenifanya nitende nini kuhusu Yesu Kristo? Mimi, mradi tu ninataka kwenda kufanya jambo hilo, liko moyoni mwangu kulifanya! Kama ... ninasema, maadamu limo moyoni mwangu kulitenda, ninakwenda kulitenda. Sheria haitaniruhusu kulitenda, ni kwa sababu ninajua ningeliadhibiwa nikilitenda. Lakini Ukweli wake hasa ni kwamba, ni wakati upendo wa Mungu ujapo moyoni mwako mpaka wewe unataka kutenda jambo Hilo. Huo ndio Ukweli wake. Kuna zile itikadi mbili. Siyo sheria au wala jambo, ama Ukalvini, yote mawili.

28 Sasa tunaona leo, pia, kuna madhehebu mengi mbalimbali. Hilo hapo kanisa Katoliki, kanisa la Kiprotestanti. Kila mmoja wao anasema wao ndio Njia, mnaona, "Tuna Njia, sisi ni Kweli." Huyo hapo Mmethodisti, anasema, "Tuna Kweli." Mbatisti anasema, "Tuna Kweli."

Vema, kwangu mimi, mradi tu wanajisikia hivyo, sivyo ilivyo, kwa sababu Yesu alisema, "Mimi ni Kweli." Mnaona?

Kwa hiyo, kama vile mahubiri yangu ya jana usiku yalivyokuwa, ya kwamba Yeye ndiye mahali ambapo Mungu aliweka Jina Lake, mahali pekee pa kuabudia. Wewe si Mkristo kwa sababu wewe ni Mprotestanti. Wewe si Mkristo kwa sababu wewe ni Mkatoliki. Wewe si Mkristo kwa sababu wewe ni Mmethodisti, Mbatisti, ama Mpentekoste. Wewe ni Mkristo kwa sababu umebatizwa katika Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu, si kwa maji. "Kuna Imani moja; Bwana mmoja; ubatizo mmoja," huo ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ubatizo wa maji unakuingiza katika ushirika. Ubatizo wa Roho Mtakatifu unakuingiza ndani ya Kristo. Hiyo hapo ile Kweli.

29 Pia tuna mawazo mawili ya hii *Ndoa na Talaka*. Sasa, kwamba, Bwana wetu ametufungulia siri ya Mihuri Saba ya Neno Lake, katika siku hizi za mwisho. Sasa, wengi wenu, hii huenda ikawa ni Kiyunani kwenu, bali kanisa langu linafahamu. Kwa kitu gani? Nawe umesikia habari za maono na yale yaliyotukia. Na swali hilo ni swali la Biblia, tumekaribishwa hapa kuamini lazima kuwepo na jibu la kweli kwa siri yote nzima iliyofichwa tangu kuwekwa misingi ya dunia. Na Biblia inatabiri na kusema ya kwamba katika siku hii siri hizi zingefunuliwa. Ufunuo 10, "Na malaika wa saba atakapopiga baragumu, mjumbe wa Laodikia, siri za Mungu zingefunuliwa." Na huu ndio wakati wa mwisho, ambao ni Laodikia.

30 Angalia ufufuo huu wote umeendelea kwa miaka kumi na mitano au zaidi, na hakuna dhehebu hata moja lililotoka kwake. Luther alikuwa na uamsho, kulitokea dhehebu; Wesley, kulitokea dhehebu; Alexander Campbell, kulitokea dhehebu; hawa wengine wote wakuu … John Smith na kadhalika, madhehebu, Moody, wakati wote. Lakini hapa kumekuwa na mmoja … Kwa kawaida uamsho huchukua tu kama miaka mitatu. Bali huu umeendelea kwa miaka kumi na mitano, na hakujatokea hata dhehebu moja, kwa maana huu ni wakati wa Mbegu. Hakuna kapi tena; baada ya kapi moja kuondoka, ni Mbegu.

Mungu yuko tayari, kama Yeye hafanyi hivyo sasa, Yeye ataliingiza Kanisa kwenye ukamilifu kwa Neno Lake, Yesu Kristo. Angalia, hapana budi kuwe na jibu mahali fulani, na likiwa Hilo, ile siri iliyotiwa muhuri saba ya Mungu, Mihuri Saba.

Ni wangapi wanaofahamu jambo hilo, inua mkono wako. Hebu tuone. Nafikiri wengi wao ni kusanyiko letu kutoka hapa karibu, sikilizeni. Kama sivyo, vitabu vitatoka hivi karibuni, juu ya somo hilo. Tuna vitabu, baadhi ya vitabu juu Yake sasa.

31 Yesu, katika somo letu, anatualika kurudi nyuma mwanzoni, kwa jibu la kweli la Kimaandiko.

Sasa, wakati alipokabiliwa na jambo hili, kulikuwa na mambo mawili yaliyoonekana. Makuhani walimwambia, "Je, mwanamume anaweza kumwacha mkewe, aoe mwingine, kwa sababu yoyote?"

Naye Yesu akasema, "Haikuwa hivyo tangu mwanzo."

Ndipo wao wakasema, "Musa alituruhusu kumpa hati ya talaka na kumwacha kwa lo lote walilotaka."

Yeye akasema, "Kwamba, Musa alifanya hivyo kwa sababu," ninaachilia hilo lishike kidogo, "kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu; lakini tangu, au mwanzoni haikuwa hivyo." Swali!

32 Swali leo, kama la amani ya ulimwengu, "Je! inakuja kwa siasa, muungano wa mataifa, yakiungana?" Nawaambia, la. Sikuzote imeshindwa, na itashindwa tena. Lakini kungali kuna jibu la kweli kwa swali hilo, "Kutakuwa na amani duniani?" Naam, dhambi itakapoondolewa duniani, kutakuwa na amani. Lakini mpaka wakati huo, hakutakuwa na amani; "Taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme." Mungu alitoa dawa ya dhambi. Sikilizeni kwa makini sasa. Mungu alitoa dawa ya kuondoa dhambi duniani, bali mwanadamu wa duniani hatakubali dawa ya Mungu.

Mungu alitupa dawa na njia ya kuwaoa wake zetu na kuishi nao, lakini mwanadamu hatakubali dawa ya Mungu, hatakubali Neno Lake juu yake. Yesu amesema jambo hili. Na hili linatukumbusha sisi kuhusu—kuhusu Maneno Yake, tukijua kwamba Yeye alisema, "Mbingu na nchi zitashindwa, zitapita, bali Langu halitapita."

33 Swali, jibu la kweli ambalo Yesu anatutaka tulirejee, ni kurejea hapo mwanzo. Halafu, hiyo ingekuwa katika *Mwanzo*, maana neno Mwanzo ni sura ya mbegu kwa kila swali katika Biblia. Na sikuzote yakubidi urejee kwenye mbegu kuona ni mbegu ya aina gani iliyomo shambani, kuona mazao yako yatakuwaje. Sasa, ni mbegu ya aina gani inayopandwa? Kitabu cha Mwanzo, kwa kuwa ndicho sura ya mbegu, tungerejea katika Mwanzo. Yesu anatutambulisha kwa Maandiko hayo, "hapo mwanzo." Sasa, kumbukeni, hapo ndipo wakati ulipoanzia. Kabla ya hapo, ilikuwa ni Umilele. Sasa, swali letu hapo lilikuwa, angalia, kama tukirejea nyuma mwanzoni.

Sasa msikose hili! Na hiyo ndiyo sababu ninataka kuzungumza pole pole, ili kwamba watu huko nje kwenye nyaya, na kwamba kanda itasema jambo hilo dhahiri.

Kama Yesu alisema, "Rudini hapo mwanzo," kulikuwako na jozi moja tu ya cho chote duniani. Kulikuwako na Adamu mmoja, Hawa mmoja, waliunganishwa na Mungu peke yake. Farasi mmoja jike, mmoja dume; kasuku mmoja wa jike, mmoja wa kiume. "Hapo mwanzo," kama alivyotuambia turudi, kulikuwa na jozi moja tu ya chochote. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Basi, tunaona sasa kwamba kila kitu hapo "mwanzo" kilikuwa kikienda katika kanuni timilifu na upatano na Mungu, hakuna kitu kilichokuwa nje ya mpangilio

Kila kitu mbinguni bado kiko katika utaratibu; nyota zote, jamii ya nyota, mfumo wa jua, kila kitu kiko katika utaratibu kikamilifu. Moja yao ikisogea, itakatiza mpango wote.

34 Sasa sikilizeni. Mnaona? Katizo moja huharibu mpango wote! Sasa, wakati wanadamu walipokuwa wakiendelea na mwendo pamoja na Mungu, pamoja na mwanamume mmoja na mwanamke mmoja, mwanamke huyu alitenda dhambi na hilo lilitupilia mbali mpango wote wa duniani kwa mwendelezo pamoja na Mungu. Kwa hiyo, neno moja lililoongezwa kwenye Kitabu hiki, ama Neno moja lililoondolewa Kwake, linamtupa Mkristo nje ya mwendelezo pamoja na Mungu, linatupa kanisa nje ya mwendelezo pamoja na Mungu, linatupa familia nje ya mwendelezo pamoja na Mungu. Kila mwamini anaweza kutupwa nje, kwa kutokukubali kila Neno la Mungu.

Halafu, mwanamke ndiye aliyesababisha kutengana kwa nyumba hiyo nzuri. Haikuwa ni Kerubi aliyeisumbua dunia. Si Adamu aliyeitupa nyumba. Haikuwa kitu kingine chochote kilichoitupa nyumba, na kutupa kitu hicho chote katika mwendelezo, bali mwanamke, Hawa. Na ni hapa ambapo "ule mwanzo," ambao Yesu alinena habari zake, ulipovunjwa. Yesu alisema, "Hapo mwanzo, Mungu alimfanya mwanamume mmoja, mwanamke mmoja, wa kila namna." Na sasa wakati mwanamke huyu … si farasi jike, si mbwa jike; lakini yule mwanamke, aliuvunja mwendelezo wote wa utendaji wa Mungu duniani, na kutupa kila kitu mautini. Mwanamke, si mwanamume, alivunja agano. Alivunja agano, kwa sababu (kwa nini?) alivuka mipaka ya Neno la Mungu. Sasa, kama alivunja agano lake na mumewe, alivunja agano lake na Mungu; basi, kwa sababu alivunja agano na Mungu, alilivunja na mumewe.

35 Na wakati unapovunja ahadi yako na agano lako kwa Neno la Mungu, hilo ndilo lililosababisha wafuasi wengi wa haramu wa kanisa, maana kundi la watu lilikusanyika pamoja na kusema, "Vema, Hilo halikumaanisha jambo *hilo*," na linatupa madhehebu yote kutokana na mwendelezo wa Neno. "Hatuamini Hilo. Daktari Jones alisema haikuwa hivyo." Lakini mradi tu Mungu alisema ni kweli, Yeye alisema, "kila neno la mwanadamu liwe uongo, na Langu liwe Kweli!" Hapo linavunja mwendelezo.

Sasa tunaona, kwa kuwa ule mwendelezo umevunjwa, basi mstari wa Uzima ulivunjwa, pia mstari wa wakati ulivunjwa, agano lilivunjwa, kila kitu kilivunjwa! Ni kitu gani kilichosababisha jambo hilo? Mwanamke. Hiyo ndiye aliyelivunja agano. Sasa, ukitaka kusoma hilo, unaweza kulisoma, Mwanzo 3.

36 Sasa, wakati huo mwanamume alifanywa kumtawala mwanamke, kwa Neno la Mungu. Hakuwa sawa naye tena. Alikuwa sawa katika maumbile, mwajua; lakini, wakati alipolivunja Neno la Mungu, Mungu alimfanya mwanamume awe mtawala juu yake. Mwanzo 3:16, ukitaka kuliandika. Hakuwa sawa tena na mwanamume. Yeye alikuwa mvunjaji wa Neno la Mungu.

Hivi hamwoni, "mwanamke," yeye, kanisa hapa chini? Mvunjaji wa Neno la Mungu, hilo lilimtupa nje kabisa katika mwendelezo. Na hivyo ndivyo kanisa limefanya, na kutupa mauti ya kiroho juu ya kitu hicho chote. Sasa mtaelewa ni kwa nini ninayagongolea mambo haya kama ninavyofanya. Ni Kweli! Huu ni ukweli wa Biblia.

Angalia, kwa nini alifanya jambo kama hili; mwanamke huyo wa kupendeza, mrembo, mkamilifu angewezaje?

Niliona picha wakati mmoja, ninaamini ilikuwa huko Ugiriki, ya msanii aliyechora picha ya Hawa. Alikuwa kitu cha kutisha sana ulichowahi kuona. Hiyo inaonyesha kile mtu wa kimwili awezacho kuangalia. Lakini, yeye hakuwa; alikuwa mrembo, maana alikuwa ni mwanamke mkamilifu, mwanamke wote.

37 Angalia, kwa nini alifanya jambo hilo, akiwa katika hali hiyo ya hali ya juu? Alikuwa sawa na mwanamume, sawa naye. Lakini sote tunajua sasa ya kwamba alipoteza usawa wake na mwanamume, wakati alipotenda dhambi, na Mungu akasema, "Mwanadamu atakuwa mtawala wako tangu hapa na kuendelea." Sasa, hayo ni Maandiko. Kama mkitaka, tungeweza kulisoma.

Ninawapa Maandiko, kwa hiyo kuokoa wakati kwa ajili ya mawasiliano haya makubwa kote nchini, mpate kuyasoma wenyewe.

Angalia sababu ya yeye kufanya hivyo. Shetani alimpataje?

Je! Ulijua Shetani alikuwa sawa na Mungu siku moja? Hakika alikuwa, kila kitu isipokuwa muumba; Yeye alikuwa kila kitu, alisimama kwenye mkono wa kuume wa Mungu, Mbinguni, yule Kerubi mkuu aliyeongoza.

Angalia sababu ya yeye kufanya jambo hili, yeye hakuwa katika uumbaji wa asili. Yeye hayuko katika uumbaji wa asili wa Mungu; yeye ni kitu kingine. Kwa hiyo, "hapo mwanzo," kama Yesu alivyorejea kwake, yeye hakuwa kiumbe asili cha uumbaji wa Mungu. Yeye ametoka kwa mwanamume, wakati Yesu aliporejea kwa hilo "hapo mwanzo."

38 Kumbuka, Adamu alikuwa wa kiume na wa kike pia, katika uumbaji wa asili, mmoja, lakini basi alitengwa kwa ubavu.

Angalia, lakini kitu kilichotoka kwa kitu kingine, na, angalia, kiumbe pekee cha uumbaji wa Mungu, cha kila mnyama na chochote kile, yeye ndiye pekee aliyebuniwa hivi. Kila jike mwingine yeyote alikuwa katika uumbaji wa asili. Kila jike mwingine alikuwa katika uumbaji wa asili, bali Hawa hakuwa katika uumbaji wa asili. Mnaona, hilo lilibidi lifanywe hivyo. Tutalifikia baada ya kitambo kidogo. Angalia, katika uumbaji huu aliokuwamo, si katika ule wa asili, bali kwa kitu kingine. Na katika uumbaji huu, kuna …

Sasa sitaki kuwaudhi, bali ninataka kuwaambia Kweli. Nawe kaa tu kimya; unafanya vizuri.

39 Hakuna kitu kilichokusudiwa kuwa danganyifu sana, kama mwanamke ambaye ni mdanganyifu. Hakuwezi kuwa na kitu kingine; hakuna kitu kilichofanyika kuwa hivyo.

Pia, hakuna kitu kinachoweza kudanganywa kwa urahisi kama mwanamke. Sasa, kule kuanguka kunathibitisha tamshi hili kuwa ni kweli, kule kuanguka hapo mwanzo.

yeye hakuwa katika ule uumbaji wa asili wa mwanzonii. Alikuwa katika Adamu, bali si katika jinsia ya kike, yeye mwenyewe, hapo mwanzo. Alitengenezwa kwa kitu kingine.

Sasa, hakuna kitu kilichoundwa ambacho kinaweza kudanganya, na kudanganywa, kwa urahisi kama mwanamke. Hakuna kitu kilichoundwa ama kinachoweza kujishusha chini kama mwanamke awezavyo. Wazia sasa. Hakuna kitu kilichoundwa, katika viumbe vyote, kinachoweza kujishusha chini kama mwanamke awezavyo. Anaweza kuurarua moyo wa mwanamume vipande vipande kirahisi kuliko kitu kingine chochote kilichopo ulimwenguni, ni mkewe. Jalia mke huyo mzuri apate kuzurura na mtu mwingine; mwangalie jamaa huyo anayeketi pale pamoja na watoto wake, machozi yakimtoka. Yeye ameumbwa hivyo. Yeye amekusudiwa kufanya jambo hili. Hakuna nguruwe, hakuna mbwa, wala mnyama mwingine, aliyeumbwa kama yeye ama anayeweza kujishusha chini awezavyo kujishusha. Sasa, hiyo ni kweli.

Kwa upande wa dada zangu, ninawatakeni tu mwangalie.

40 Hakuna mnyama anayeweza kuwa mzinzi. Mnamwita mbwa "malaya," mbwa jike, mnamwita dume … nguruwe "jike," bali uadilifu wake ni maili milioni moja zaidi ya nyota wengi wa Hollywood. Hivyo ndivyo alivyobuniwa kushuka chini. Hawezi … Wazia tu jambo hili sasa. Hakuna kitu ulimwenguni, kilichoumbwa katika uumbaji wa Mungu, ambacho kinaweza kuwa cha uzinzi, kikishuka chini namna hiyo.

Unasema, "Ngoja kidogo, 'jamani'!" Tutalifikia hilo. Mwanamke hana budi kusema "ndiyo."

Angalia, hakuna kitu kilichoundwa kushuka chini sana, ama kuwa kichafu, ila mwanamke. Mbwa hawezi kufanya hivyo, nguruwe hawezi kufanya hivyo, ndege hawezi kufanya hivyo. Hakuna mnyama asiye mwadilifu, wala hawezi kuwa, kwa kuwa yeye hajabuniwa apate kuwa hivyo. Nguruwe jike hawezi kukosa uadilifu, mbwa jike hawezi kukosal uadilifu, ndege jike hawezi kukosa uadilifu. Mwanamke ndiye kitu pekee anayeweza kufanya hivyo.

41 Sasa mnaona mahali Shetani alipoenda? Mnaona? Lakini bado anao, yeye ndiye aliye na nguvu za kusema "ndiyo" au "la." Mnaona, inategemea mahali anapotaka kujishikilia. Mnaona? Sasa hapa tunaweza kuona dhahiri uzao wa nyoka, mahali ulipoingia. Kuna mahali pamoja tu ambapo angeweza kwenda. Kama hilo halingelidhihirisha kabisa, basi mtu fulani ni kipofu. Mnaona? Mnaona, ilibidi iende kwenye jambo hilo.

Angalia, sababu ambayo wanyama hawakuweza kufanya hivyo, mnyama wa kike, walikuwa katika uumbaji wa asili. Lakini mwanamke huyo hakuwa katika uumbaji huo wa asili. Sasa tunarudi kuchimba hili, kisha tutawaleta moja kwa moja kwenye siku za kisasa, katika Agano.

Yeye ameumbwa, peke yake, kwa ajili ya uchafu na maisha machafu. Mbwa hawezi, wala mwanamke mwingine hawezi. Ni mwanamke tu anayeweza. Mbwa au wanyama wengine wo wote, mara moja kwa mwaka, na hilo ni kwa ajili ya watoto wake; si kwa ajili ya anasa za kujuana kimwili, bali kwa ajili ya watoto wake. Yule nguruwe jike wa kale, yule mbwa koo wa kale, mara moja kwa mwaka, mara moja, hiyo ni kwa ajili ya watoto wake. Bali mwanamke ameumbwa kwa ajili ya wakati wo wote anaotamani. Nimeyafutilia mbali baadhi mambo fulani hapa sasa; unaweza kuwazia yaliyobakia. Mbwa hawezi; mwanamke anaweza. Ninatumaini ya kwamba Roho Mtakatifu atawafunulia mengine yaliyobakia niliyofutilia mbali hapa.

42 Yeye ndiye pekee, jamii ya kike, ambaye amefanywa mrembo kuliko wa kiume. Hakuna kiumbe kingine miongoni mwa kitu chochote. Viumbe vingine vyote vya Mungu ni madume warembo, kama vile katika wanyama, ndege, na kadhalika, daima dume ni mrembo.

Mwangalie yule kulungu mkubwa, pembe kubwa nzuri, kiumbe maarufu; na maskini jike mdogo, mnyenyekevu. Angalia jogoo mkubwa pamoja na manyoya yake yote mazuri; na maskini kuku, kahawia. Waangalie ndege, jogoo na kuku. Mbona, kwa nini ikawa hivyo, miongoni mwa viumbe vyote vya Mungu? Kila kiumbe, wa kiume ndio wanaovutia sana. Kati ya kondoo, kati ya—wa nguruwe, kati ya farasi, kati ya kitu kingine chochote, daima ni dume mkubwa aliye mzuri, na katika ndege.

Lakini katika jamii ya binadamu, mwanamke ndiye mrembo, si mwanamume; kama yuko, kuna kasoro fulani, kuna mbegu iliyochanganyikana mahali fulani. Kiasili ndivyo ilivyo. Kwa nini, kwa nini ilifanywa hivyo? Kudanganyia. Mbunifu wake, Shetani, angali anamtengeneza, pia, katika siku hizi za mwisho.

43 Hebu nisimame hapa kwa muda kidogo tu. "Mrembo!" Je! Ulijua, kwenye maangamizi ya kwanza, kimataifa, ya ulimwengu, ama ulimwenguni kote, ilikuwa ni kwa sababu ya wanawake warembo? "Wana wa Mungu walipoona binti za wanadamu ni wazuri, wakajitwalia wanawake." Hiyo ni kweli?

Umeona ongezeko la urembo wa wanawake katika siku hii? Nimeona picha ya Pearl O'Brien, ambaye alipaswa kuwa mwanamke aliye mrembo kuliko wote nchini, wakati mmoja. Hakuna msichana tineja katika shule hii ambaye hangemzidi, tukinena ya urembo.

Kuongezeka kwa uzuri wa wanawake kunaonyesha wakati wa udanganyifu. Ni lini kanisa lilionekana rembo zaidi kuliko lilivyo leo? Kila kitu kinaonyesha majengo makubwa mno na mazuri, na mamilioni ya *hiki* na mamilioni ya *kile*. Hivi hamwoni, "mwanamke," udanganyifu!

44 Sasa, hakuna kitu kinachoweza kujishuka kama yeye, naye ameundwawa ili aweze kuwa mdanganyifu. Naye Shetani kweli anamfanyia kazi leo, katika siku hizi za mwisho, kwa sababu yeye ndiye mbuni wake. Ninaweza kuthibitisha jambo hilo sasa. Rudi moja kwa moja hapo mwanzo, ni nani aliyeanza kumfanyia kazi, Adamu au Shetani, Mungu ama Shetani? Mnaona, huyo ndiye mbuni wake. Ni silaha yake kuu kumtupia mwanamume kwenye uchafu wake, akiwa ni mwanamke mrembo, anaweza kumshawishi mwanamume kwa njia yo yote anayotaka. Ndugu, si klabu karamu cha chang'aa chini hapa ambacho humnasa mwanamume; ni huyo mwanamke mrembo anayetembea mitaani, hatua za madaha, nusu uchi. Hilo ndicho kiwezacho… Huyo ni yule mdanganyifu papo hapo. Naye ni hatari sana kwake, hatari kabisa. Unaweza kuniuliza juu ya Shetani kuwa ndiye mbuni wake, bali hiyo ni Kweli. Shetani alimtengeneza. Yeye angali anafanya hivyo.

45 Hebu niwaonyeshe jambo fulani katika Maandiko. Sina budi kuwarudisha kwenye Maandiko, nanyi mtoe maoni yenu mnapoyaangalia leo.

Shetani ndiye anayeonyesha urembo wa aina hiyo. Kama tutaona, yeye alikuwa ndiye mrembo kuliko Malaika wote Mbinguni. Hiyo ni kweli? Naye alitaka kuifanya Mbingu mahali pazuri zaidi kuliko ufalme wa Mikaeli. Hiyo ni kweli? Pia, kuonyesha ya kwamba Kaini alikuwa ni mwanawe, alitoa ibada nzuri zaidi, akapamba madhabahu yake kwa matunda na maua, na kadhalika. Hiyo ni kweli? Mrembo! Dhambi ni nzuri, tunayoita urembo leo. Na dhambi ni danganyifu, kwa uzuri. Kamwe usingemwangalia mwanamke anayeshuka kwenda barabarani na kusema yaliyo moyoni mwake. mnaona? Lakini nilitaka kusema mambo haya kusudi muone ni kwa nini Shetani ndiye mbuni wake. Hiyo ni kweli kabisa, mwanawe mwenyewe alithibitisha jambo hilo, Kaini. Sasa, yeye ni mrembo kusudi aweze kudanganya.

46 Ulimwengu ni mzuri hivyo unaweza kudanganya. Ninamaanisha *kosmos*, utaratibu wa ulimwengu. Ni mzuri sana kwamba unaweza kudanganya, mahali pazuri sana na anasa.

Kumbukeni nabii, Amosi, wakati alipokuja na kuangalia chini mjini, na kuiona kama Hollywood ya kisasa, maskini macho yake madogo yakawa madogo zaidi, chini ya nywele hizo za kijivu zikining'inia usoni mwake. Alishuka akaenda kule na Ujumbe, na akautangaza kwa nguvu mahali pale. Yeye alisema, "Mungu yule yule mnayemdai kumtumikia, atawaangamiza!" Hiyo ni kweli.

Dhambi inapendeza. Wanamfikiria Yuda kama mlevi fulani mzee nje hapa mtaani mahali fulani, mwenye kinywa chenye inzi kimening'inia, na kadhalika, kuwa ni Yuda. Yuda alikuwa mzuri wa sura, mwenye nguvu, mdanganyifu. Si huyo jamaa aliye karibu nawe, si mtu huyo (mzee mkulima) anayeingia akiwa amevaa ovaroli, usimjali huyo akiwa karibu na mkeo; ni yule mtu mjanja, yeye ndiye mlagai.

Dhambi inapendeza machoni pa ulimwengu, lakini Mungu hadhihirishwi katika urembo wa namna hiyo. Je! Ulijua jambo hilo? Mungu hudhihirishwa katika tabia, tabia ipendezayo.

47 Katika Biblia, Isaya 53, kama unataka kuandika Maandiko. Ina milolongo ya Maandiko iliyoandikwa kando yake hapa kwa ajili yake. Isaya 53, Biblia ilisema juu ya Bwana wetu Yesu, ya kwamba, "Hakuwa na uzuri hata tumtamani. Nasi tulimficha nyuso zetu." Hiyo ni kweli? Hatukumtamani, kwa sababu Yeye hakuwa sura nzuri. Labda alikuwa ni jamaa mdogo, mwenye mabega yaliyoinama, mwekundu, wala hakupendeza kuwa kiongozi. Yeye hakuonekana kama kiongozi. Alizungumza lugha ya mitaani, na kadhalika, kama watu wafanyavyo, watu wa kawaida, kwa hiyo basi Yeye hakuonekana kama Yeye alikuwa mwanachuoni maarufu, mwenye elimu, mzuri, aliyevalia joho, na kila kitu. Yeye alikuwa ni Mtu wa kawaida tu. "Hakukuwako na uzuri katika Yeye, hata tukamtamani." Aliingia na kutoka miongoni mwa watu, moja kwa moja, hata hawakujua Yeye alikuwa ni Nani. Yeye hakuonekana kama mungu akitembea, kile tungefikiria kuwa ni mungu. Lakini, hata hivyo, Yeye alikuwa hivyo!

48 Je! Uliona wakati Bwana Mungu aliposema na—na Samweli, "Nenda nyumbani kwa Yese ukamtie mafuta mmoja wa wanawe, mfalme, achukue mahali pa Sauli"?

Sasa, watu walimchagua Sauli, wakati Samweli aliwaambia kabisa wasifanye hivyo. Yeye alisema, "Mungu hataki muwe na mfalme; Yeye ni Mfalme wenu." Kisha akasema, "Je! Nimewahi kuwaambia jambo lo lote, katika Jina la Bwana, ila lile lililotimia? Je! Nimewahi kuwaomba pesa au kitu fulani, kingine, kwa ajili ya riziki yangu?"

Wao walisema, "La, hukuwahi kamwe kutuomba pesa. Na cho chote ulichosema, katika Jina la Bwana, kilitimia. Lakini tunataka mfalme, hata hivyo," kwa hiyo wakamchagua Sauli. Angalia kile ulimwengu ulichochagua! Angalia kile Israeli walichachagua! Israeli, hao wenye upako wa Mungu, walimchagua mtu ambaye tangu mabega yake kwenda juu alikuwa mrefu kuliko mtu ye yote nchini; jamaa mkubwa mno, mtu mzuri na mwenye sura nzuri, naye sikuzote alikuwa ni tatizo kwao.

Lakini Mungu alisema, "Nitawachagulieni mfalme nimpendaye Mimi." Kwa hiyo Yeye akasema, "Samweli, sitakuambia yeye ni nani, bali wewe panda uende kule. Yeye ni mmoja wa wana wa Yese.

49 Ndipo Yese, mkewe, na hao wote wakaangalia huku na huko, kasema, "Naam, mwana wetu wa kwanza, yeye ni mtu mkubwa, mrefu, mwenye sura nzuri, ataonekana sawa tu kwa taji ya mfalme. Yeye ni mwerevu. Yeye amesoma. Yeye ni mtu mzuri. Ninajua atakuwa sawa kabisa. Anatamka maneno yake barabara."

Walipomleta, Samweli akachukua chupa ya mafuta na kumwendea. Akasema, "La, Bwana alimkataa." Kwa hiyo akashuka akaenda zake, kwa wana sita, na Bwana akamkataa kila mmoja wao. Akasema, "Je! Hakuna mwingine?"

"Loo," akasema, "naam, yupo mmoja, yuko huko nje akichunga kondoo. Yeye huketi tu kule nyuma na kucheza nyimbo, na kuziimba, na kupiga makelele, na kuendelea. Lakini, yeye ni maskini jamaa mdogo aliyeinama mabega, mwekundu, hatafaa kamwe kuwa mfalme."

Akasema, "Nenda kamlete." Na wakati Daudi alipokuja mbele za nabii, nabii alikimbia na mafuta na kuyamwaga kichwani mwake, kasema, "Huyu ni mteule wa Mungu." Si mrembo; bali tabia. Mungu huangalia tabia.

50 Mwanadamu huangalia uzuri wa asili. Ni danganyifu. Na hiyo ndiyo sababu mwanamke alipewa urembo huo, kwa udanganyifu, apate kudanganya. Mwanamke mrembo, kama yeye hautumii kwa njia sahihi, ni laana kwake; huo utampeleka yeye haraka kuzimu kuliko kitu cho chote nijuacho. Kama yeye … Kama anaweza kuwa mrembo, hakika, mradi tu anakaa na mumewe na kufanya yaliyo mema, na hilo—hilo ni zuri na bora. Bali anaweza kuchukua kitu kile kile na, jamani, jinsi anavyoweza kudanganya nacho, kwa kuwa alipewa kufanya hivyo.

Angalia, sasa, lakini Mungu anadhihirishwa katika tabia. "Yesu hakuwa na uzuri wa kumtamania," lakini hapajawahi kuwa na utu kama Wake, duniani.

Sasa tunaona, leo, ya kwamba m—mhusika wa kanisa, Shetani na kundi lake, wanaangalia makanisa makubwa, mazuri, mambo mazuri. Hivyo ndivyo ulimwengu unavyoangalia leo. "Loo, ni mchungaji, wakati maarufu *fulani*, na *fulani*, kasisi kweli kweli na mcha Mungu, anatoka akiwa na majoho yake makubwa, na mambo kama hayo." Wanamwita mrembo huyo.

Lakini watakatifu halisi wa Mungu hutafuta tabia ya Neno lililothibitishwa.

Hivyo ndivyo watakatifu walivyofanya katika siku hiyo, walipomwona Yesu. Yeye hakuwa kitu cha kuangalia, bali waliona Mungu alikuwa ndani Yake. Waliona Mungu alikuwa pamoja Naye.

51 Hivyo ndivyo ambavyo hao, Yoabu na hao watu pamoja na Daudi, maskini jamaa mdogo, bali waliona yule—yule mtu alikuwa ndani yake. Waliona ya kwamba Mungu alikuwa ndani yake, nao walijua angeingia mamlakani siku moja. Wao … Mmoja aliwaua hao ndugu wengine watano wa Goliathi, akiwa peke yake. Mwingine aliwauwa watu mia tatu; wakati baadhi ya wanawake walikuwa wakichuma maharagwe ya chakula cha mchana, na jeshi lilikuwa limeenda zake, naye alichukua mkuki na kuua watu mia tatu, Wafilisti. Tabia! Kwa nini? Walikaa karibu na Daudi. Walijua upako ulikuwa juu yake, nao walijua alikuwa akiingia madarakani.

Picha safi ya Kanisa leo ambalo litasimama na Neno! Tunajua hilo litathibitishwa. Tunajua Hilo litapata mamlaka siku moja. Ingawa Sauli … Naye alikuwa mkimbizi kutoka mataifa mengine, lakini walijua atatawala. Tunajua Yeye anaingia madarakani, pia, kwa hiyo tunalichukua Neno hilo na kusimama papo hapo, haidhuru linagharimu nini. Kama itatubidi kuwakata Wafilisti, ama kurukia shimoni na kumwua simba, kama vile mtu mmoja alivyofanya, tunaenda kwa vyo vyote, maana ni … hivyo ndivyo Mungu alivyopanga iwe. Tunatafuta tabia.

52 Sasa unaweza kuniuliza, "Kwa nini Yeye alimruhusu yeye atengenezwe namna hii?" Sitaki kuchukua wakati mwingi sana, maana nina mengi zaidi ya kusema hapa. "Kwa nini," swali linaweza kutokea basi, "kwa nini Mungu alimfanya mwanamke huyu namna hii? Kwa nini alimruhusu awe hivyo?" Ilikuwa kwa ajili ya mapenzi Yake Mwenyewe. Hakika.

Sasa kama ukitaka kufungua katika Biblia yako kwa dakika moja, hebu na tufungue Warumi 9, kwa dakika moja tu, na kuwaonyesha jambo fulani, jinsi Mungu anavyofanya mambo haya, kama ukitaka ku—kuyasoma. Nasi tunaweza kuona hapa yale Mungu anayofanya kwa mapenzi Yake Mwenyewe. Warumi 9:14.

> *Tuseme nini basi?*
>
> *Kuna udhalimu kwa Mungu? ...*

Wakati Yeye alipomchagua Esau, au alipomchagua Yakobo na kumkataa Esau, kabla ya mmoja wa wavulana wote wawili kuweza kuwa na haki ya kuchagua, mwenyewe, wala mmoja wao; kabla hawajazaliwa, wangali katika tumbo la uzazi la mama yao, Mungu alisema, "Namchukia Esau, na nampenda Yakobo." Mnaona? Kwa nini?

> *Maana amwambia Musa, Nitamrehemu yeye nimrehemuye, nitamhurumia yeye nimhurumiaye.*
>
> *Basi, kama ni hivyo, si ... katika uwezo wa yule atakaye, wala ... wa yule apigaye mbio; bali wa yule arehemuye, yaani, Mungu.*
>
> *Kwa maana maandiko yasema juu ya Farao, ya kwamba, Nilikusimamisha kwa kusudi hili, ili nionyeshe nguvu zangu kwako, jina langu likatangazwe katika nchi yote.*
>
> *Basi, kama ni hivyo, ... (sasa angalia hapa) ... kwa kuwa yeye ... atakaye kumrehemu humrehemu, na atakaye kumfanya mgumu humfanya mgumu.*

*Basi*, wewe ... *utaniambia , Mbona* basi yeye ... *akilaumu? Kwa maana ni nani ashindanaye na kusudi lake?*

*La! Sivyo, Ee binadamu; wewe u nani umjibuye Mungu? Je! Kitu kilichoumbwa kimwambie yeye aliyekiumba, Kwani kuniumba hivi?*

*Je! Mfinyanzi hana mamlaka juu ya udongo, kwa donge lile lile la kufanya chombo kimoja cha heshima, na hicho kingine cha aibu?*

*Ni nini basi, ikiwa Mungu kwa kutaka kuonyesha ghadhabu yake, na kuudhihirisha uweza wake ... uvumilivu mwingi, alichukuliana na vile vyombo vya ghadhabu vilivyofanywa tayari kwa uharibifu;*

*… ili audhihirishe wingi wa utukufu wake katika vile vyombo vya rehema, alivyovitengeneza tangu zamani vipate utukufu;*

53 Sasa bishane na Hilo kwa muda mfupi. Mungu alifanya hivyo! Ilimbidi kulifanya namna hiyo. Ilibidi liwepo. Sasa sikilizeni sasa kwa karibu dakika tano, ninataka kuvuta usikivu wenu kwa jambo fulani.

Mungu ni nini? Mungu ni Umilele mkuu. Hapo mwanzo, huko nyuma kabisa kabla hakujawa na mwanzo, Yeye hata hakuwa Mungu. Je! Ulijua jambo hilo? Mungu ni "kitu cha kuabudiwa," wala hakukuwa na kitu cha kumwabudu. Aliishi peke yake.

Na ndani Yake mlikuwamo sifa. Sifa ni nini? Wazo. Sasa utapata kitu ambacho kinahusiana na somo la usiku wa leo. Angalia, Yeye alikuwa sifa Zake zilizokuwa ndani Yake. Sasa, ilikuwa ndani Yake kuwa Baba, ilikuwa ndani Yake kuwa Mungu, ilikuwa ndani Yake kuwa Mwana, ilikuwa ndani Yake kuwa Mwokozi, ilikuwa ndani Yake kuwa Mponya. Na mambo haya yote hapa yanaonyesha tu sifa Zake. Hakuna kitu kilicho nje ya utaratibu. Unafikiri Mungu hakuona mwisho tangu mwanzo? Hakika, Yeye alifanya hivyo. Hakuna kitu kilicho nje ya utaratibu, ni kuonyesha tu sifa Zake.

54 Sasa, Yeye asingeweza kuwa mwenye *haki* na kumfanya mtu kuanguka. Ilimbidi kumweka sawa, kwa uhuru wa kuchagua, kufanya chaguo lake mwenyewe, bali akijua angeanguka.

Sasa, Yeye hawezi kuwa Mwokozi isipokuwa kitu fulani kipotee. Yeye hawezi kuwa Mponya isipokuwa kitu fulani ni kigonjwa. Mambo haya yalipaswa yawe hivyo. Mungu aliwaumba hivyo kusudi sifa Zake kuu ziweze kuonyeshwa. Kama hakungekuwa na jambo hilo, Yeye kamwe asingekuwa Mwokozi. Lakini tunajua Yeye alikuwa, hata kabla hakujakuwa na wakati, Yeye alikuwa Mwokozi. Yeye alikuwa Mwokozi, kwa hiyo hapana budi kuwe na kitu kilichopotea. Itakuwaje?

Kama akikichukua na kukipoteza, kusudi tu akiokoe, basi si haki kwa hukumu Yake. Asingeweza kumpeleka mtu kuzimuni, na awe mwenye haki. Yeye ni mwema, mpole, mkweli, mwaminifu, Naye ni Hakimu mkuu. Mnaona, Yeye angekuwa akifanya kazi dhidi Yake Mwenyewe.

Kwa hiyo ilimbidi amweke mtu nje hapa, na kumfanya awe na uhuru wa kujichagulia, kusudi apate, akijua, apate kuanguka; na mtu huyo, katika mfano Wake Mwenyewe, angewezaje kuanguka? Sasa mnaona Nuru ya mchana? Kwa hiyo, ilimbidi atengeneze kitu kilichotoka kwa kingine, kitu fulani kutoka kwenye kile cha uumbaji wa asili. Sasa mnaona jambo hilo. Mnaona? Hilo ndilo jambo lenyewe. Mnaona? Halafu, hicho ndicho kilichoanguka. Yeye alikifanya, akijua kingeanguka. Na kimewekwa mikononi mwa Shetani, kama chombo kisicho na heshima. Heshima imewekwa wapi leo? Fikirini juu ya jambo hilo. Angalia kwa makini sasa.

55 Halafu tena, kusudi layeye kuundwa namna hii na sio kama majike wengine, kwa nini mwanamke kuundwa hivyo na sio majike wengine? Hakuna hata mmoja wa hao majike wengine aliyebuniwa namna hiyo. Hawako hivyo, leo. Hawawezi. Kwa kuwa hajaumbwa jinsi hiyo, hawezi kufanya hivyo. Kwa nini Yeye hakumfanya huyu mwanamke basi, mwanamke, kama tu majike wengine, ili awe hivyo tu, angeweza tu kuwalea watoto wake? Ndipo angempata mumewe, na kuishi; na ifikapo wakati mtoto wa wake, angempata mtoto wake. Mbona, mbona hakumfanya hivi?

Siwezi kusema maneno haya. Nanyi mnaelewa yale ninayonena, sivyo? Kama unaweza kuelewa, sema "amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Naam. Mnaona? Kuna wasichana wadogo wanaoketi hapa, na wavulana wadogo, mnaona. Lakini unajua, mnyama hana budi kufikia wakati fulani wa mwaka, na mwenziwe, basi hivyo tu yatosha. Lakini, mwanamke, ni wakati wowote. Na kwa nini alimfanya hivi?

56 Sasa angalia mpango Wake mkuu ukifunuliwa, tunapoendelea kupitia hapa sasa, mkamilifu kabisa jinsi tuwezavyo kuwa. Sikujua jambo hili mpaka hivi majuzi.

Kwa nini hakumfanya hivyo hapo mwanzo, kama majike Wake wengine? Kwa sababu isingekuwa desturi Yake. Yeye ni Chemchemi ya usafi wote. Hiyo ndiyo sababu ilimbidi Yeye kumwachia Shetani ampate, jambo lile yeye alilotenda katika upotovu. Kiumbe kama hicho kingekuwa, hakingemfaa Yeye, jinsi kilichokusudiwa hapo awali kuwa.

Kazi Zake zote alizobuni, katika ile ya asili, ziko katika mwendelezo. Kazi Zake zote za asili zilikuwa katika mwendelezo. Mbwa jike, mbwa dume; mnaona, ng'ombe jike, ng'ombe dume; kila kitu katika mwendeleo. Maumbile yote yako katika mwendelezo. Mbegu hufa, zinaingia ardhini; ni kama tu mauti, kuzikwa, kufufuka. Utomvu hushuka chini kutoka kwenye mti, unaangusha jani lake, unarudi tena mwaka ufuatao na ufufuo wa jani jipya. Mnaona ninalomaanisha? Kila kitu, hata maumbile, ya Mungu, yote yako katika mwendeleo, katika umoja; na hapa pana mmoja aliyetengenezwa nje ya mwendeleo wa Mungu. Maumbile yamebuniwa sana hivi kwamba hayawezi kutenda dhambi. Wazia! Uumbaji wa asili, wa Mungu, usingeweza kutenda dhambi.

Loo, hivi hamlioni sasa, katika mtazamo huu hapa, upotovu wa kanisa? Ya asili ni Neno la Mungu! Hakuna dhambi katika Mungu. Mnaona ninalomaanisha? Hiki hapa kiumbe kilichopatikana kwa upotovu. Mungu atakuwa na Kanisa, lakini angalia kitu hiki kilichopotoshwa walicho nacho hapa nje.

Mungu ana wa kiume na wa kike. Lakini, mwanamke huyu, mnaona, dalili zake hasa zinaonyesha kile kilichokuwa katika nia ya Mungu. Tungeweza kuchukua saa moja, ama mbili, na kulivunjavunja hilo. Yeye … Akakifanya kiumbe hiki kwa njia hiyo, Yeye alikifanya kiumbe hiki kisha akakiachilia ili Shetani aweze kukipata, naye akakipata. Angali naye bado. Afadhali angekimbilie Msalabani, kama mwanamume, pia.

57 Angalia, maumbile yote yako katika mwendelezo. Kama angalimfanya mwanamke katika uumbaji ule ule wa asili, kusingekuwako na dhambi, kwa sababu asingeweza kufanya hivyo, asingeweza kufanya hivyo. Yeye ni upotovu wa uumbaji wa asili.

Vivyo hivyo dhambi yote ni upotovu wa Kweli ya asili! Uongo ni nini? Ni Kweli iliyopotoshwa. Uzinzi ni nini? Ni tendo sahihi lililopotoshwa. Kwa hiyo kuna kiumbe kilichopotoshwa, hicho hapo kitu kizima kilichopotoshwa. Na hilo jambo zima linatamkwa kwa herufi d-h-a-m-b-i, imekaa pale pale. Hiyo ndiyo sababu swali ni kubwa sana.

Kipande tu, kipande kidogo, kilichofanywa kwa mwanamume, kumdanganya; Mungu alikifanya, imethibitishwa papa hapa. Hilo ndilo kusudi la kumfanya mwanamke.

Mwanamke mzinzi ndiye kitu cha chini kabisa kinachoweza kufikiriwa, duniani. Samahani kwa jambo hili, enyi wasichana. Yeye si kitu ila pipa la binadamu la takataka, maonyesho ya zinaa. Hivyo ndivyo tu alivyo, mwanamke mzinzi, ni pipa la uchafu wa zinaa za binadamu, ambamo vinyaa, uchafu, upotovu, na vinyaa vya hali ya chini sana huandaliwa naye. Ni kwa nini ameumbwa kwa njia hii? Kwa ajili ya udanganyifu. Kila dhambi iliyowahi kuwa duniani ilisababishwa na mwanamke.

Na mchambuzi aliyetoka Chicago hivi punde, mwa—mwanamke aliandika nakala hii, kikosi cha polisi; kwamba walifuatilia, Marekani, katika miji ya Marekani, kwamba "Asilimia tisini na nane ya kila uvunjaji wa sheria ambao uliwahi kutendwa katika Marekani, kulikuwa aidha na mwanamke ndani yake au nyuma yake."

Sasa ninasema haya yote, kufikia jambo moja hapa mwishoni, ili kwamba mwone kuna shida gani.

58 Alifanywa apate kudanganya, kama alivyomfanya Adamu hapo mwanzo, kumwambia ya kwamba tunda hilo lilikuwa la kupendeza, na kadhalika, kumdanganya na kumwondoa kwenye Neno. Hivyo ndivyo kanisa linavyofanya siku hizi, jambo lile lile.

Lakini basi, baada ya hilo, akawa mtawala wake, apate kumtawala.

Sasa ni tofauti jinsi gani katika siku hii, katika siku hii ya mawazo. Badala ya yeye kuwa mtawala wake, yeye amekuwa mungu wake. Hakika, anamtawala. Sasa labda mnaweza kufahamu vizuri kile nimekuwa nikipinga. Kwa urembo wake na kwa utawala wake wa zinaa umbo lake alilopewa na Shetani, uundaji wa pembeni ambao aliufanya Shetani, ametumwa kuwadanganya wana wa Mungu. Naye anaweza kuwapeleka kuzimuni zaidi ya chombo chochote alicho nacho Shetani. Hiyo ni kweli kabisa.

Ninazungumza juu ya wasio waadilifu sasa, si ninyi akina dada. Tutakupa mahali pako, mahali panapofaa, katika dakika chache, katika Neno la Mungu hapa. Ilikuwa katika mpango wa Mungu tangu mwanzo—mwanzo.

59 Sasa kufanya hivi leo, mungu wa Marekani ni nini? Mnakumbuka katika Maskani miaka mingi iliyopita, nilihubiri juu ya jambo hilo? Mungu wa siku hizi za kisasa, maskini kipusa anayeketi pale akiwa amejipodoa, na nguo ameivuta juu ya magoti yake, na mambo kama hayo. Nikasema, "Tazama mungu wenu!" Na hiyo ni kweli, yeye yuko kwenye kila tangazo, nusu uchi. Yuko mitaani, vivyo hivyo.

Ni chombo cha Shetani, "tangu mwanzo," Yesu alisema. Mnaona? Tunaona ya kwamba ndivyo ilivyo sasa, na "tangu mwanzo," na yale Yeye anayozungumzia.

Sasa, makafiri walikuwa wakimfanya yeye mungu, (mlijua jambo hilo?) mungu wa kike. Hakika walikua. Wanamfanya mungu wa kike, kwa maana walifanya tendo la zinaa katika ibada zao. Walidai ya kwamba, "Yeye alikuwa ndiye muumba. Katika tumbo lake la uzazi alichukua mbegu na kuumba." Huo ni

uongo. Kuna Muumba mmoja tu, huyo ni Mungu. Lakini mnamkumbuka Paulo pale? "Diana, wa Efeso," sanamu ya mwamba, kasema, "mungu wa kike wa Mbinguni, aliyetupwa chini." Hivi hamwoni jinsi ibada za kikafiri zilivyo?

Nasi, bila kujua, tunarudi moja kwa moja kwenye ibada za kipagani tena, kwa wanawake, kiumbe cha chini sana duniani, ibada ya wanawake! Atamshawishi mwanamume kwa njia yo yote anayotaka. Na bila kujua, uzuri huo wote kwa nje, ya kwamba kuzimu iko ndani. Sulemani alisema, "Yeye, malango yake ni malango ya kuzimu."

60 Sasa tunaona dhahiri hapa yale Yesu aliyonena katika Ufunuo, sura ya 2 na aya ya 15, ya fundisho la Unikolai, kuja kwa kanisa hilo kujiondoa kwenye Neno.

Pia tunaweza kuona hapa, waziwazi, vipindi hivi vichafu, vya kikafiri, vichafu tulivyo navyo kwenye televisheni, vya malkia wa zinaa wa Hollywood. Tunaweza kuona uchafu wa mji huu, wakati watoto hawa, maskini wasichana wadogo wakitembea huku na huku mtaani hapa, wakiwa na nguo ndogo sana, zilizobana, wakizunguka—zunguka, na kulikuwa na baridi ya kutosha kuwagandisha hadi kufa. Hawajui ya kwamba huyo ni ibilisi anayefanya hivyo. Wao wana pepo wachafu, wala hawajui! Huoni mbwa jike akifanya hivyo, sivyo? Huoni jike jingine lo lote likifanya hivyo, na afadhali mtu mume ye yote asimwendee, hata hivyo.

61 Mnaona, sasa mnapata picha? Tutaanzisha jambo fulani katika dakika moja, Bwana akipenda.

Sasa mnawaona Wanikolai, mnaona fundisho lao.

Unawaona visura matineja, wanavyowaita, hawa wenda uchi mtaani. Walizoea kwenda kwenye maonyesho fulani machafu pembeni, kutazama mwanamke akivua nguo. Fungueni tu macho yenu, angalieni barabarani, hivyo tu ndivyo mnavyopaswa kufanya sasa. Kitu hicho chote ni kuvua nguo. Hakika. Wanalitenda kwa sababu gani? Kutamanisha, kubemba, hicho ndicho kitu pekee anachoweza kufanya. Yeye hufanya hivyo kwa sababu yeye ni mchafu. Yeye hufanya hivyo kwa sababu ameumbwa hivyo. Yeye hatambui ya kwamba yeye ni chombo mikononi mwa Shetani, na hivyo ndivyo alivyo.

Hata katika shule zetu leo, wanafundisha matendo ya kujuana kimwili. Ulimwengu wetu uliooza wa ibada za wanawake! Ninajua hawataki kuamini jambo hilo. Wanasimama na kuimba wimbo fulani, na kadhalika, siku moja; na kuondoka kwenda na wanawake, kuzururazurura, usiku kucha. Mnaona? Vema. Wakati, mbele za Mungu, Neno, yeye ndiye mnyama wa chini sana kuliko wanyama wote ambao Mungu aliwaweka duniani. Angalia.

62 Hiyo ndiyo sababu Mungu anamkataza kufundisha Neno Lake. Hiyo ni kweli. Timotheo wa Kwanza 2: 9-15, "Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, au kujitwalia mamlaka yo yote." Mnaona? Na pia Wakorintho wa Kwanza 14:34, "Wanawake wenu na wanyamaze katika makanisa, maana hawana ruhusa kunena; pia yanena Torati nayo." Lakini, leo, kanisa linafanya nini? Wanawafanya wachungaji, wainjilisti, wakati Biblia kata kata inakataza jambo hilo. Na Biblia ilisema, "kama vile Torati inenavyo nayo," kulifanya liende katika mwendelezo, jambo hilo lote.

Kama tu alivyokuwa Mwana-Kondoo, usiku uliopita, mahali pekee pa kuabudia, chini ya Damu iliyomwagika ya Mwana-Kondoo. Ni mahali pekee leo, katika Kristo. Njia pekee unayofanya ni kuingia ndani Yake. Hapo ndipo mahali pekee pa kuabudia. Daima ilikuwa hivyo. Mahali pekee pa kuabudia ni chini ya Damu iliyomwagika.

63 Kwa hiyo sasa tunaona picha nzima ya jambo hilo ikifunuliwa kwetu. Huyo hapo. Hiyo ndiyo sababu Mungu hatamruhusu kufundisha, hatamruhusu afanye chochote kanisani ila kuketi kimya na uso uliofichwa.

Sasa mnaweza kuona ni kwa nini nimesema mambo na kufanya mambo ambayo nimefanya, nikijua haya yote moyoni mwangu, ndugu, dada? Ninajua, akina dada, mimi … mna nafasi yenu (kwa muda mfupi tu), na tabia nzuri sana ambayo Mungu anaweza kuumba ndani yenu. Lakini ninajaribu kuzungumzia upande ule mwingine, kuonyesha hasa "mlivyokuwa mwanzoni." Yesu alitwambia "rudini mwanzo," kuchunguza hilo. Hivyo ndivyo tunavyofanya.

Sasa imenibidi kugonga sehemu muhimu katika mengi ya mambo haya, nami natumaini mtaelewa hilo. Nanyi watu ambao mtakuwa mkisikiliza kanda hii, natumaini mnaelewa. Rudini tu. Ni kuonyesha tu ya kwamba Yesu alisema, "Rudini, mwanzo, mkachunguze." Mambo yote, rudini mwanzoni. Mnaweza kuona, leo.

64 Mbona, watu, wao wanasema mimi ni mchukia wanawake. Hiyo ni mbali na Kweli. Siwachukii. Wao wananiita, "Mchukia wanawake!" Kumbuka, walimwita Paulo mchukia wanawake. Mhudumu mwanamke, si muda mrefu uliopita, alisema, "Loo, wewe ni kama mzee Paulo, yote aliyofanya ni kutuonea sisi wanawake."

Mtakatifu wa Mungu, aliyeruhusiwa kuandika Biblia, Agano Jipya, na mnapinga Maneno yake? Yeye alisema, "Kama Malaika kutoka Mbinguni atafundisha kitu kingine cho chote zaidi Hiki ambacho nimenena, na alaaniwe," licha ya mhubiri fulani mwanamke.

Walisema Eliya alikuwa mchukia wanawake. Yeye hakuwa mchukia wanawake, wanawake halisi. Yeye hakuwapenda tu hao Mayezebeli.

Na kama hivyo ndivyo ilivyo, basi haina budi kuwa Mungu hana budi kuwa vivyo hivyo, kwa maana Yeye ni Neno lililowajia manabii. Kwa hiyo haina budi kuwa ni Mungu, vivyo hivyo, kwa hiyo, mnaona, Yeye anajua uumbaji wa asili, "tangu mwanzo," Yeye alisema, "tangu mwanzo." Walikuwa manabii ambao Neno liliwajia.

65 Naye alimfanya kuwa mwanamume, na si mwanamume kwa ajili yake. Je! Ulijua jambo hilo, ya kwamba, "Mwanamke aliumbwa kwa ajili ya mwanamume, na si mwanamume kwa ajili ya mwanamke"? Ni wangapi wanaojua jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Biblia inafundisha jambo hilo. Vema. Alipewa mahali fulani katika mwanamume, kabla ya kule kuanguka, kuwa sawa juu ya maumbile yote. Lakini "baada ya" kuanguka, sasa hapa tunaleta somo. Bali "baada ya" kule kuanguka, yeye alikuwa mtawala wake, sharti anyamaze katika mambo yote, sasa baada ya ule mwanzo wa asili kupita.

Yesu alisema, "Tangu mwanzo haikuwa hivyo." Hapo ndipo wakati ulipoanza, wakati Mungu alipoufanya kwanza katika uumbaji Wake wa asili. Wote wanaofahamu, semeni "amina" tena. [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Hapo mwanzo Mungu aliumba mwanamume mmoja na mwanamke mmoja. Lakini basi mwanamke huyo alifanywa tofauti na wanyama, wanyama wengine wote, kwa ajili ya udanganyifu. Sasa angalia sasa, "Haikuwa hivyo tangu mwanzo." Aliumbwa, kama angekaa katika hali ya asili, asingesababisha kamwe anguko lo lote. Lakini yeye alisababisha kuanguka na usumbufu ambao ulivunja mwendelezo wote wa Mungu, na kutupa mauti, huzuni, na cho chote kile, duniani. Alifanywa hivyo.

66 Sasa tazama sasa "baada ya" mwanzo, baada ya mwanzo, baada ya wakati kuanza; nyuma huko ulikuwepo Umilele, umekwisha. Angalia, baada ya anguko hilo kufanywa na Hawa, baada ya kule kuanguka, kulikuwa na haja ya kufanywa agano lingine. Sasa hili litawakwaza, bali nitawapa Maandiko kuthibitisha ya kwamba hii ni Kweli. Sasa angalia baada ya anguko, Yesu alisema … Mungu, hapo mwanzoni, alikiumba kimoja cha kila aina; bali sasa, baada ya kuanguka, sasa tunavuka hapo. Agano hilo lilikuwa sawa; lakini sasa, baada ya kule kuanguka, kuna agano lingine lililofanywa. Sasa yeye hakuwa mtawala tena pamoja naye, kila mmoja hana budi kuwa na agano tofauti.

67 Sasa hebu tuone kama hiyo ni kweli. Hebu na tuchukue Mwanzo 3, na tuone kama hii ni kweli, sasa tunapoendelea, maana tunataka kuwa na hakika ya mambo haya, yanafundishwa na kuoneshwa kweli kabisa. Ili kwamba papa hapa tuwe na wakati mchache, maana hatuko mbali sana na mwisho sasa, kufikia sehemu ya mwisho ya somo, kuonesha ni kwa nini na vipi kuhusu talaka, na kadhalika. Sasa katika Mwanzo sura ya 3, nasi tutaanza sasa na kifungu cha 3, na cha 16. Hebu tuanzie kwenye aya ya 14.

> *Bwana Mungu akamwambia nyoka,* (sasa ataenda kumlaani), *Kwa sababu u—-umeyafanya hayo, umelaaniwa wewe kuliko wanyama wote, ... na kuliko hayawani wote walioko mwituni; kwa tumbo utakwenda, na mavumbi utakula siku zote za maisha yako;*
>
> *Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino.* (Ile ahadi, "atakuja kupitia kwa mwanamke," yule Masihi, kukomboa.)
>
> *Akamwambia mwanamke, …*

Sasa angalia, sasa hilo hapo agano na yule nyoka. Ambapo, wote walikuwa sawa kabla, hapo mwanzo, ama kabla ya mwanzo.

> *Akamwambia mwanamke, Hakika nitakuzidishia uchungu wako, na kuzaa kwako; kwa utungu utazaa watoto; na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala,* (Wao si sawa tena.)

Sasa yeye amegeuka moja kwa moja, naye ndiye mtawala.

> *Akamwambia Adamu, Kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nalikuagiza, nikisema, Usi ... yale; ardhi imelaaniwa* (si Adamu amelaaniwa, sasa) *ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako;*
>
> *Michongoma…na miiba itakuzalia; nawe utakula mboga za kondeni;*
>
> *Na kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.*

68 Maagano mawili. Sasa hilo linafunga "mwanzo," wa yale Yesu aliyosema, "Haikuwa hivyo hapo

mwanzo." Tuna agano lingine sasa. Angalia, ni agano lingine. Sasa kuna agano kwa kilichoumbwa, na kilichotolewa kwa kilichoumbwa. Angalia, kuanguka kulileta shida, mauti, kwa kila kiumbe cha uumbaji, ikifanya tofauti katika maumbile yote. Sasa hebu na tuone yale Yesu alisema kuhusu, "tangu mwanzo haikuwa hivyo." Sasa sivyo ilivyo "tangu," sasa ni "baada" ya mwanzo. Sasa kuna agano maradufu.

Kwanza lilikuwa ni agano tu, Adamu na Hawa walikuwa sawa, mwanamume mmoja na mwanamke mmoja. Sasa yule mwanamke alitenda dhambi, na (anafanya nini?) ambayo iliwatupa wote mautini, na ilimbidi Mungu kufanya agano kwa hilo, agano lingine. Hili hapa papa hapa katika Mwanzo 3:16, Yeye alifanya agano lingine.

69 Sasa ulimwengu utajaa watu, si kwa uumbaji wa asili wa Mungu, kama vile hapo mwanzo, si kwa uumbaji wa asili, bali kwa tamaa ya kujuana kimwili. Sasa hilo linashughulikia "mwanzo," sivyo? Hapo mwanzo kulikuwepo na mwanamume mmoja na mwanamke mmoja, kimoja cha kiume na kimoja cha kike; bali hapo alipovuka msitari ule na kuleta dhambi hii, sasa ulimwengu wabidi ujazwe watu tena, kwa kujuana kimwili, sio kwa uumbaji; kwa kujuana kimwili. Mnaona mahali mwanamke huyo alipo sasa, sasa? Lakini hivyo ndivyo ulimwengu ulivyo na watu siku hizi, kupitia kwa wanawake.

Hiyo ndiyo sababu ilibidi Yesu aje kwa njia ya mwanamke, kuirudisha kwenye mwanzo wake wa asili tena, bila tamaa ya kujuana kimwili. Yeye amezaliwa na bikira. Lakini, haleluya, utakuja wakati ambapo haitakuwa tena kujuana kimwili, lakini Mungu ataita watoto Wake toka kwenye mavumbi ya ardhi, iwe kama ilivyokuwa hapo awali, si kwa njia ya mwanamke ye yote; lakini kwa kufinyanga udongo na nuru za ulimwengu, na petroli, Yeye ataumba tena kama alivyomfanya Adamu mara ya kwanza. Yesu alilifanya hilo liwezekane, kwa njia ya Mungu kujifanya Mtu na kuja ulimwenguni kusudi apate kufa, kupitia mwanamke huyu. Sasa ni wakati wa kujaribiwa, kwa dhambi.

70 Sasa mnaona basi, "baada ya" mwanzo, ilikuwa ni kitu kingine kilichoingizwa. Sasa hili litawashtua. Je! Umechoka? [Kusanyiko linasema, "La." — Mh.] Keti tu kimya kwa muda kidogo tu.

Basi agano maradufu lilipofanywa na mwanamume na mwanamke, kwa kujuana kimwili, agano jingine kabisa (si lile agano la hapo awali, bali agano jingine), sasa nini kinaingizwa? Kuoa wake wengi, kwa jumla. Ndipo, baada ya mwanzo, kuoa wake wengi kulíletwa katika mwanadamu na katika wanyama pia; baada ya mwanzo, kule kuanguka. Mungu sasa, anaweka asili mpya tena, iliyo hafifu, kwa kujuana kimwili. Mungu aliumba wa kwanza bila jinsia. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Sasa ni agano jingine na maumbile, Yeye huliweka katika utaratibu mwingine, kwa kujuana kimwili. Agano la pili: mwanamume mmoja, wanawake wengi; dume mmoja wa kulungu, kundi zima la jike. Hiyo ni kweli? Fahali mmoja, kundi zima la ng'ombe, ng'ombe; jogoo mmoja, kuku wengi. Hiyo ni kweli? Daudi mmoja, aliyeupendeza moyo Wake, akiwa na wake mia tano; na watoto mia moja waliozaliwa kwake, katika mwaka mmoja, wa wanawake mbalimbali, mtu aliyeupendeza moyo Wake Mungu. Sulemani mmoja, akiwa na wake elfu. Lakini angalia sasa, haikuwa hivyo hapo mwanzo, lakini sasa ni "baada" ya mwanzo. Mwanamke amefanya jambo hili, basi anakuwa kile alicho sasa. Mnaona?

71 Daudi, mfalme aliyemwakilisha Kristo! Shikilia hilo moyoni mwako. Daudi alimwakilisha Kristo. Unaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Kristo anaketi … ataketi kwenye kiti chake cha enzi. Na huyu Daudi, mtu aliyeupendeza moyo wa Mungu Mwenyewe, alikuwa na wake mia tano. Mnaona ninalomaanisha? Daudi pamoja na wake zake mia tano, Sulemani pamoja na elfu yake. Na Sulemani ni mwana wa Daudi, kimwili; ambaye anamwakilisha Yesu Kristo, Mwana wa Daudi, kiroho. Lakini hayo ni maisha ya kawaida, maisha ya kujuana kimwili. Haya yatakuwa kiroho, yaliyoumbwa. Kwa nini? Yameumbwa. Mnaona, hivyo ndivyo ilivyokuwa hapo mwanzo, bali si sasa katika maisha haya tunayoishi sasa.

Angalia, msikose jambo hili sasa, chukueni yote mioyoni mwenu. Lakini hakuna hata mmoja wa hao wanawake angeweza hata kuwa na mume mmoja zaidi. Mwanamume ndiye kiumbe cha asili, si mwanamke. Hakuna hata mmoja wa hao wanawake angeweza kuwa na mume mmoja zaidi, bali huyo mume mmoja angeweza kuwa na wake elfu. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni Biblia. Sasa nimerejea nyuma, nikachukua wakati wangu na nikawaonyesha nyuma huko kile kilichoanza, yale aliyosema Yesu. Sasa mnaliona dhahiri? Wangeweza kuwa na wengi …

72 "Loo," unasema, "hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya Israeli tu." Ndivyo?

Wakati Ibrahimu alipomchukua Sara kwenda katika nchi ya Wafilisti, kulikuwako na mfalme kule chini jina lake Abimeleki. Naye Sara alikuwa na umri wa miaka mia moja, moja kwa moja kwenye jambo hilo, bali alikuwa amebadilishwa akawa mwanamke kijana na akafanywa mrembo. Mnajua jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Vema. Naye Abimeleki alimtaka awe mke wake. Mnakumbuka Ujumbe wangu juu hilo? Abimeleki alitaka kumchukua Sara awe mkewe. Pengine alikuwa na wake chungu nzima, lakini asingeweza kumchukua kama ameolewa na Ibrahimu. Kwa hiyo Ibrahimu akamwambia Sara, "Sema kwamba wewe ni, 'ndugu yangu,' kwa sababu ataniua ili aweze kukutwaa." Kwa nini hakumfukuza Ibrahimu nje ya nchi, na kumchukua mke wake na kuendelea? Haikuwa tu sheria waliyokuwa nayo waamini, bali ilikuwa kwa watu wote katika uumbaji. Mwenye dhambi au mtakatifu, unawajibika, ewe

mwanamume, kwa matendo haya. Huyo hapo mfalme kafiri. Ni wangapi wanaojua hadithi hiyo ni kweli? ["Amina."] Ni Biblia, Mwanzo, yapata sura ya 16, nafikiri.

73 Mnaona, Abimeleki angemchukua awe mkewe. Yeye alijitayarisha kumpata msichana huyu mpya wa Kiebrania. Naye akasema, "Huyu ni ninii yangu …" Akasema, "Huyo ni ndugu yangu."

Akasema, "Huyo ni dada yangu."

Ndipo Abimeleki akasema, "Nitamchukua tu awe mke wangu basi." Ungeweza kuwazia mtu akifanya jambo kama hilo? Lakini yeye alifanya hivyo.

Na halafu usiku huo, wakati akienda kulala, Bwana alimtokea katika ndoto, na kusema, "Abimeleki, wewe ni kama mtu aliyekufa." Yeye alikuwa analinda huo, huo ukoo wa damu ya Kiyahudi pale, mnaona. Yeye alisema, "Wewe ni kama mtu aliyekufa. Una mke wa mtu mwingine unayetaka kumwoa."

Akasema, "Bwana, unajua unyofu wa moyo wangu." Kasema, "Hivi yeye hakuniambia huyo alikuwa ni 'ndugu' yake? Si yeye mwenyewe alisema, 'Huyo ni dada yangu'?"

Akasema, "Najua unyofu wa moyo wako, hiyo ndiyo sababu nisingekuruhusu unitende dhambi Mimi." Hiyo ni kweli? Kasema, "Mrudishe mkewe, kwa sababu mtu huyo ni nabii Wangu. Na usipomrudisha mke wake … Na umwache akuombee, sio kasisi wako. Asipokuombea, taifa lako lote limekwisha." Amina. Kuna neema ya ajabu. Sawa. "Taifa lako lote limeangamia. Huyo ni mke wa mtu huyo, naye ni nabii Wangu." Amina. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hayo ni Maandiko. Sawa.

74 Sasa tunaona, mauti yalisababishwa. Mauti chanzo chake ni dhambi ya mwanamke, yalikuja kwa njia ya mwanamke na sio mwanamume. Kwa njia yake ya kuishi maisha yake, na kwa yeye, mauti yote yanakuja. Njia yake ya kutoa uhai ni mauti. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Ayubu 14, kama unataka kuandika Maandiko.

Ninayo, kama ukihoji jambo hili, ninayo Maandiko yaliyoandikwa kwa kila fungu la haya.

Kama ukitaka kusoma Ayubu 14 hapo, inasema, "Mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke siku zake za kuishi si nyingi, naye hujaa taabu." Hiyo ni kweli? "Yeye huchanua kama vile ua, kisha kukatwa, likaharibika," na kadhalika. Mnaona? Kila mtu aliyezaliwa na mwanamke, amezaliwa katika mauti mara tu alipokuja.

Lakini wakati anapozaliwa katika uumbaji wa Mungu, hawezi kufa; yeye anatoka kwenye ule Mti mwingine uliokuwa katika bustani ya Edeni, Kristo. Uzima wa Milele huja kwa Mti huo.

"Loo," unasema, "alikuwa ni mti?" Hakika. "Vema, walisema, 'Usile matunda ya mti huu.' Mungu alisema, katika Mwanzo huko nyuma, 'Usile matunda ya mti huu.'"

Mbona, mwanamke ndiye mti. Yeye ndiye mti wa matunda. Wewe ni tunda la mama yako. Tunda la tumbo la uzazi ni wewe. Hiyo ni kweli. Na halafu tunda la Mti wa Uzima, lililokuwa katika bustani ya Edeni, ni Kristo. Kupitia kwa mwanamke mauti ilikuja; kupitia kwa yule Mtu, katika uumbaji wa asili, kukaja Uzima. Kuzaliwa na mwanamke ni mauti; kuzaliwa na Kristo ni Uzima. Unalipata wazo hilo? Hapo ndipo. Sasa mnaona mahali miungu wa kike walipokwenda, sivyo?

Kwanza Adamu na Hawa waliwakilisha Adamu na Hawa wa pili, mnaona, kule kuongezeka. Sasa kule kuongezeka kwa Adamu na Hawa kulikuwa kwa njia ya kujuana kimwili, kuijaza dunia, lakini haikuwa hivyo hapo mwanzo. Mungu aliumba tu mwanamume na mwanamke, kama alivyofanya kwa viumbe Vyake vingine, mnaona, kisheria, kama tu Kanisa.

75 Sasa hebu na sisi, kwa sababu ya Kweli hizi za Mungu zilizothibitishwa, tutafute zaidi kidogo, kama ukitaka. [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Vema. Sasa hili linaweza kuumiza kidogo tu mpaka tutakapofikia kilindi chake, lakini nitawaonyesha tu Ukweli wake.

Hakuna mhudumu anayeweza kuoa mjane. Je! Ulijua jambo hilo? Mnataka kusoma hilo? Vema, ingia katika Walawi, Mambo ya Walawi 21:7 na Ezekieli 44:22, na itakuonyesha ya kwamba ukuhani haukupaswa kuoa mwanamke aliyeguswa na mwanamume. Mfano huu ni wa Bibi-arusi bikira wa Yesu Kristo, kwa sababu waliushughulikia ule Moto wa Mungu, makuhani walifanya hivyo, wana wa Haruni. Hatuna wakati wa kusoma hayo yote, na kutoka ifikapo adhuhuri, tungali tuna dakika ishirini. Na hao ni wana wa Haruni ambao walishughulikia Moto wa—wa—wa Mungu, kwa hiyo wasingeweza kuoa mwanamke aliyekuwa ameguswa na mwanamume mwingine. Mungu asiyebadilika alisema hivyo. Hawangeweza kuoa mwanamke mwingine, na mwanamke aliyeguswa na mwanamume, ikionyesha kwa mfano hapa, kama unataka kuliona, kwamba Kanisa la Mungu aliye hai ni Neno safi la Mungu lisilighoshiwa, na sio madhehebu ambayo yameshikwa-shikwa na binadamu.

76 Angalia, hebu na tusome hili hapa. Ninataka kuwaeleza jambo hili. Mathayo 5, Yesu alinena hapa juu ya jambo ambalo ni muhimu sana. Tunataka kuona jambo hilo, Mathayo 5. Niliandika juu ya …

Niliweka bayana baadhi ya mambo niliyokuwa nikitaka kumwambia mtu huyo tu, kwa hiyo nilikuwa na muda kidogo sana kuyasema mbele ya dada zetu. Lakini ninataka ku—kwenda hapa sasa kabla …

Sasa, dada, ninataka kukuweka mahali ambapo Neno la Mungu lilikuahidi, na unaona basi unakaa mahali hapo, pia.

Mathayo 5:32. Ninawatakeni mwone hapa, kuunga mkono wazo hili hili la "mmoja" na "wengi." Mathayo, thelathini- … Nafikiri ni Mathayo 5:32, 31 kwanza.

> *Imenenwa pia, Mtu akimwacha mkewe, na ampe hati ya talaka;*

Huyo ni Yesu akinena, Yeye alisema, "tangu mwanzo." Sasa angalia.

> *Lakini mimi nawaambia, Kila mtu amwachaye mkewe, isipokuwa ... kwa habari ya uasherati, amfanya kuwa mzinzi; na mtu akimwoa yule aliyeachwa, azini; …* (Ona) *kila mtu amwachaye mkewe, isipokuwa kwa sababu ya uasherati, amfanya uzinzi:* (kwa nini? Ataolewa tena) *na kila amwoaye yule aliyeachwa, azini.*

77 Mnaona, yeye ana mume aliye hai, kwa hiyo hakuna mwanamume anayeweza kumwoa. Sijali anafanya nini na yeye ni nani, ana mume aliye hai, hakuna sababu kwake kuolewa tena kamwe. Lakini, sivyo, kwa mwanaume. "Husababisha mwanamke," si mwanamume. Mmelipata? Inakubidi kulifanya Neno liendelee katika mwendelezo. Mnaona, hakuna kitu kisemacho mwanamume asingeweza, lakini mwanamke hawezi. Mnaona, "humfanya mwanamke," si mwanamume. Hivyo ndivyo hasa Biblia inavyosema, "humfanya." Haikunenwa dhidi ya mwanamume kuoa tena, bali "mwanamke." Kwa nini? Kristo katika mfano.

Angalia, imeelezwa ya kwamba hawezi kuoa tena, ila bikira tu. Anaweza kuoa tena. Yeye anaweza, anaweza kuoa tena kama ni bikira, bali hawezi kuoa mke wa mtu mwingine. Hakuna hakika. Na kama akimwoa mwanamke aliyeachwa, anaishi katika uzinzi, sijali yeye ni nani. Biblia ilisema, "Kila mtu amwoaye mwanamke aliyeachwa, anaishi katika uzinzi." Haya basi, sio hao waliotalikiwa.

Mnaona ile ya asili huko nyuma, "tangu mwanzo," sasa? Kuoa tena, sasa angalia, anaweza, bali mwanamke hawezi. Kama vile Daudi, kama Sulemani, kama mwendelezo wa Biblia nzima, sasa, kama vile Daudi na hao wengine.

78 Sasa mnaona katika Wakorintho wa Kwanza 7:10, angalia, Paulo anaamuru mke ambaye, ambaye anamtaliki mumewe, akae peke yake au akapatanishwe, sio kuolewa tena. Yeye hana budi kubaki peke yake, ama apate kurudiana na mumewe. Hawezi kuolewa tena. Hana budi kubaki peke yake, lakini, angalia, yeye hakusema juu ya mwanamume huyo. Mnaona, huwezi kulifanya Neno linene uwongo. "Tangu mwanzo," sheria ya kujuana kimwili kwa kuoa wanawake wengi. Sasa, Neno la Mungu linapatana na maumbile ya Mungu, liko katika mwendelezo.

Mnaona vile kuna itikadi moja ilienda mashariki, na nyingine ikaenda magharibi, kwenye jambo hilo? Huna budi kurudi kwenye ile Kweli, upate kujua ni nini.

Imekuwa hivyo daima, hilo ndilo agano la kawaida na Mungu tangu mwanzo. Kwanza, kabla ya mwanzo, tangu mwanzo kulikuwa tu na mmoja kwa mmoja. *Baada ya* dhambi kuingia, ndipo kulipokuwepo na mwanamume mmoja na kundi la wanawake; inakwenda hivyo katika maumbile, kila mnyama, na wanadamu na mwili wa kawaida ni mnyama. Sisi tu jamii ya wanyama wanyonyeshao watoto wao, tunajua hivyo, sisi sote, mnaona, na yote ni maumbile ya Mungu katika mwendelezo.

79 Lakini sasa kwa kuwa ile Mihuri imefunguliwa, Roho wa Kweli anatuelekeza kwenye Neno. Hilo linaelezea kwa nini makosa yote yamekuwepo katika nyakati zote, kwa sababu zile Muhuri hazikuwa zimefunguliwa, Hili halikuwa limefunuliwa. Ni kweli.

Angalia, wewe, huwezi kuvifanya vivuli visidhihirike. Kama nilivyowahubiria usiku uliopita kuhusu kivuli kuvuka sakafu, kinapaswa kije sawa. Yawezekanaje kuwe na kivuli cha ndovu kikija kupita kwenye sakafu, ndipo pandikizi la mtu mwembamba liwe ndilo yule ndovu, au yule ndovu kuwa ndiye pandikizi la mtu mwembamba?

Sasa, hebu uliangalie katika mfano halisi.

Sasa, kuna mwanamke wa kweli, mwanamke wa kweli, bikira, ambaye huolewa na mumewe, na anaishi, naye ni kitu kilichobarikiwa kwa mwanamume. Kama Mungu angaliweza kumpa mwanawe kitu bora zaidi kuliko mke, Yeye angempa hicho.

Lakini ametengenezwa awe wa kutamanisha, na hakuna kiumbe kingine duniani kilichotengenezwa namna hiyo. Hakuna kiumbe kingine duniani kilichotengenezwa namna hiyo. Hiyo ndiyo sababu unaona kule kuoa wanawake wengi, kwa sababu ya jambo hilo. Huko ndiko kulikoliingiza.

80 Sasa angalia, katika mwisho, angalia, kuna Yesu Kristo mmoja (hiyo ni kweli?), Mtu mmoja, Mungu, Imanueli. Unaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Lakini washiriki wa Mke wake ni wengi, mnaona, maelfu mara maelfu (hiyo ni kweli?), Mke Wake, Bibi-arusi, Kanisa. Mnaelewa sasa? ["Amina."]

Hiyo ndiyo sababu Yeye alimwambia Adamu, kabla kujuana kimwili hakujaletwa au kuingizwa, "Ongezekeni, mkaijaze nchi," wakati yeye bado alikuwa katika mwanzo, wakati alipokuwa bado vyote viwili wa kiume na kike yeye mwenyewe. Hapo, inaonyesha basi kwamba Bibi-arusi yabidi atoke kwenye Neno, kwa ongezeko la kiroho, kuongezeka, mnaona, kuijaza nchi.

81 Sasa katika kitendo cha zinaa, mnaona, zile itikadi zimevichanganyisha vitu hivyo viwili. Kwa hiyo huwezi kufanya hivyo, huna budi kuirudisha kwenye Ukweli wake, "hapo mwanzo."

Na hatimaye kutakuwepo na Bwana Yesu mmoja, na Bibi-arusi Wake wengi, umoja. Mnalipata? Kulikuwa na Daudi mmoja kwenye kiti cha enzi kimoja, mfalme mmoja (aupendezaye moyo wa Mungu) na wake mia tano. Yesu akiketi kwenye Kiti Chake cha Enzi, haleluya, katika ule Utawala wa Miaka Elfu, pamoja na Mke; kama ilivyokuwa hapo mwanzo, aliumbwa kutoka duniani, kwa mkono wa Mwenyezi Mungu, katika ufufuo, wa washiriki wengi. Haya basi.

Enyi wanawake, jitahidini kuwa hivyo, njoni katika Kristo, ndipo hamtakuwemo katika takataka za uchafu ule nje kule. Bali maadamu wewe ni mshiriki tu wa kanisa ukijaribu kuishi maisha maadilifu na mazuri, wewe mwenyewe, hutafaulu. Wala mtu hawezi kufanya jambo hilo nje ya Kristo. Kama vile Paulo alivyoendelea kusema, "Lakini wako katika Kristo, hakuna mwanamume wala mwanamke." Wote ni mmoja.

82 Bali kuifanya hii *Ndoa na Talaka* iwe sawa, kusudi mpate kujua ni lipi lilikuwa sahihi na lipi lilikuwa ni kosa, sasa Yeye anaonyesha dhahiri hapa katika mifano hii. Kuna Kristo mmoja; na washiriki wengi wa Mke huyo. Angalia, Yeye anaweza kutuacha kwa ajili ya uasherati wa kiroho na mafundisho ya uongo, wakati wo wote atakao; lakini unawezaje kuthubutu kumwacha, na kuupata? Mwanamume anaweza kumwacha mkewe na kuoa mwingine; bali si mwanamke kumwacha mumewe na kuolewa na mwingine. Mnaona vivuli vyote na vielelezo pale vimewekwa sawa kabisa? Unaona ule uumbaji wa asili; sio kiumbe kilichotoka kwa kingine mahali po pote. Si kanisa; Bibi-arusi kupitia Neno. Si mwanamke; mtu huyo, kila wakati. Hiyo ndiyo sababu kamwe halineni neno lo lote dhidi ya mwanamume kutenda jambo hilo; sikuzote ni mwanamke. Hiyo ni kweli kabisa.

Bali anaweza kuwa Bibi-arusi wa Kristo, kwa kuwa … Na kumbuka, yeye akiwa sehemu ya mwanamume, Biblia ilisema anaweza ku- … "Hata hivyo simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kutwaa mamlaka yo yote, bali awe katika utulivu. Kwa maana Adamu aliumbwa kwanza, na Hawa baadaye. Wala Adamu hakudanganywa, lakini kiumbe kilichotolewa kwa kingine kilidanganywa. Walakini ataokolewa *kama* akiendelea katika utakaso na moyo wa kiasi, na kuzaa watoto, na yote hayo," kwa sababu basi hapo anakuwa sehemu ya mwanamume huyu. Hilo ndilo linaloleta …

83 Kwa nini Ibrahimu haku … Kwa nini Mungu hakumuua Sara akiketi pale pale, akikana, na akisema uongo papo hapo mbele ya Mungu? Akiketi pale kama Mwanadamu mwenye mwili uharibikao, akila mkate, akinywa maziwa, Naye akasema, "Kwa nini Sara alicheka nyuma kule upande wa nyuma," nyuma Yake, katika hema, Yeye hakuwa amemwona huyo mwanamke, "akisema hivi, 'Yawezekanaje mambo haya'?"

Akasema, "Sikusema hivyo kamwe!" Aha loo, jamani, mwambie Mungu ya kwamba Yeye ni mwongo, mbele za Zake? Bali asingeweza kumchukua. Kwa nini? Yeye ni sehemu ya Ibrahimu. Amina. Asingeweza kumdhuru bila kumdhuru Ibrahimu.

Sasa ninyi wanawake mnaona mahali penu. Na Biblia ilisema, "Enyi wanawake iweni kama Sara alivyokuwa, ambaye alijipamba kwa mavazi ya kujisitiri, akaishi kwa uaminifu na wa kweli kwa mumewe, akimpenda yeye kiasi kwamba (mumewe) yeye alimwita 'Bwana" wake, mtawala, mwenye umiliki.

84 Na ninyi, baadhi yenu wanawake, mnavaa nguo hizi chafu na kutoka nje hapa kujianika mbele za wanaume. Yesu alisema, "Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake." Basi ni nani aliye na hatia, yule mtu ama wewe? Yeye ni wa kiume, aliyeumbwa ili aweze kutekeleza tendo hili, mnaona; nawe ni wa kike, unayepaswa kukataa.

Na kwa nini unajiweka nje namna hiyo? Siyo kwa ajili ya starehe, unajua haiwezekani, huku unakuwa nusu maiti kwa baridi unapovaa kaptura. Mnaona, haiwezi kuwa ni faraja. Basi ni kitu gani? Ni kwa ajili ya uchafu! Hutakubali jambo hilo, bali Biblia inasema hivyo. Ni Kweli. Ni roho mchafu aliye ndani yako. Hutaki kuwa mchafu; bali hutambui, kiroho wewe ni mchafu, kwa sababu unajionyesha mwenyewe kuwa ni mchafu.

Sasa, mwanamume, magoti yake mazee, machafu na yenye mafundo, na kama karibu hakuwa na nguo zo zote kamwe, isingeleta tofauti yo yote, mwili wake hautamanishi. Kwa nini? Yeye alikuwa katika uumbaji wa asili, tabia; Inapaswa kuwa hivyo, mnaona. Lakini, wewe ulitolewa kwa mwingine, ukatamanishe.

Mungu, uturehemu! Loo, jamani, ulimwengu huu wenye dhambi! Nitafurahi utakapokwisha.

85 Tazama, Yeye anaweza kumwacha mke Wake wakati wo wote apendao, lakini mkewe hawezi kumwacha; Yeye anaweza kunifanya mimi, Yeye anaweza kunitupa mavumbini wakati wo wote anapowazia kunitupa, bali, loo, ndugu, afadhali kamwe nisijaribu kumtupa Yeye pale, nimekwisha.

Sulemani angeoa mwanamke ye yote ambaye hakuwa ameloewa, angeoa mwanamke ye yote aliyetaka. Kuhani angeweza kuoa tu mwanamke aliyekuwa bikira. Sulemani …

Kama vile Daudi, alioa (jina lake lilikuwa nani?) Abigaili. Ambapo, kulikuwa na mtu aliyeitwa "mpumbavu," alikuwa na mke mzuri, naye akafa. Naye Abigaili alikuwa amemwoa Daudi; yeye alikuwa ni mfalme, si kuhani, mnaona, kwa hiyo a—alioa.

Lakini kuhani asingeweza kufanya hivyo, kwa sababu amemkaribia au alichukua mwanamke kuwa mke wake ambaye tayari alikuwa mke wa mtu mwingine. Kwa hiyo hiyo inaonyesha ubikira wa Kanisa la Bwana Yesu Kristo, itambidi Bibi-arusi kuwa asiyeghoshiwa, Neno, pasipo hata Neno moja kukosekana mahali po pote. Hakika. Ungeweza kuwazia bibi-arusi halisi, titi moja limeng'olewa, na, jingine, lina kasoro, unajua? Huyo hatakuwa Bibi-arusi wa Kristo. Yeye ni mkamilifu. Yeye ni kila kitu ni Neno, hakuna hata Neno moja likishindwa po pote. La.

86 Angalia, Yeye anaweza kumwacha, bali mwanamke huyo hawezi kumwacha. Yeye alifanya hivyo, na akalithibitisha, katika siku ambapo Luther, Wesley, na Pentekoste, walipokataa kuendelea kuwa sehemu Yake kwa kufanya mapenzi ya kiroho kusudi wapate mimba ya sehemu zaidi ya Neno. Mnaelewa? Alikataa. Kanisa la Kiluteri lilikataa Kristo awe na tamaa zaidi kwake; Luther alikataa. Na hebu niseme hivi, mtaniita mimi kitu haidhuru; hivyo ndivyo ilivyo leo kwa kila moja yao, yanashindwa kulitwaa Neno, yanamkataa Kristo!

Na mwanamke ye yote ambaye anamkatalia mwanamume mtoto wake, hapa haki kuwa mke kwake. Amina. Mnakumbuka, katika Biblia, wakati mfalme alipomwoa Esta? Kwa sababu malkia alikataa, alijipatia mwingine tu. Na wakati ninii … Ilikuwaje wakati yeye alipokataa kutoka panoja na mfalme na kumtii? Ni jambo lile lile kwa mwanamke ambaye anakataa kuwa mke wa mumewe.

87 Na ndivyo ilivyo kwa kanisa linalokataa kupata mimba katika wakati tunaoishi sasa, kuzaa watoto wa wakati huu. Sisi si Waluteri, sisi sio Wawesley, wala sisi si Wapentekoste! Hatuna budi kuwa watoto wa wakati huu, kupitia mimba ya Neno la Mungu, kumzaa Mtoto wa wakati huu, Mtoto wa Mbegu. Amina. Natumaini mnafahamu. Hangeweza kupata mimba, la, kwa hiyo Yeye alifanya nini? Akamwacha, katika talaka. Hiyo ni kweli. Lakini mkewe asithubutu kumwacha. Yeye alimwacha.

Yeye aliendelea kulifunua Neno Lake kwa ule Mwili, na kumthibitisha, yule yule, Yeye Mwenyewe. Watoto Wake wameanza kwa namna fulani kufanana na Yeye, kwa sababu Hilo linakomaa sasa kabisa, au, wanakuwa wana wa Neno, sio wana wa kanisa. Watoto wa Neno! Na Bibi-arusi atakuwa Bibi mdogo wa Neno, anayependeza, asiyeghoshiwa, asiyeguswa na dhehebu la mtu ye yote, nadharia yo yote iliyoundwa na binadamu. Atakuwa ni Bibi-arusi wa Neno asiyeghoshiwa kabisa! Amina na amina! Natumaini mtalipata hilo, hewani. Atakuwa binti wa Mungu aliyepata mimba.

88 Mnaona jinsi mwanamke anavyoweza kuwa na heshima kuu? Waona jinsi kanisa linavyoweza kuwa kitu kikuu sana, lakini mnaona ambako uchafu umelifikisha? Halafu ukijaribu kulinganisha kanisa hilo huko nje na Kanisa hapa, huwezi kufanya hivyo. Halafu kujaribu kulinganisha kanisa lile nje kule na Kanisa hapa, huwezi kufanya hivyo.

Kwa nini kuna mambo kama hayo? Ni sheria ya Mungu, sheria ya kulinganisha. Tutajuaje jinsi ya kufurahia mchana kama hakukuwa na usiku? Tutajuaje jinsi ya kufurahia hali ya hewa kavu kama hakukuwa na mvua? Tungejuaje kumfurahia na kumheshimu mwanamke halisi, kama hakungekuwa na mchafu?

89 Aliendelea kulifunua Hilo, kulifunua Neno Lake, lakini kuna mtu kati yetu anayethubutu kumwacha Yeye na kuolewa na mwingine.

Sasa hakika bila shaka ni kwa nini nadharia zote mbili zimekosea. Huwezi kulifanya liende *hivi*, limekwenda; ukilifanya liende *vile*, litaenda hata lipite ile ahadi. Hii hapa ahadi, hili hapa jambo papa hapa. Neno halijipingi. Halina budi kukaa katika mwendeleo sasa, si zaidi ya vile Mathayo 28:19 isivyopingana na Matendo 2:38.

Sasa, baadhi yenu wanawake, baadhi yenu wanaume, na—najua ham—hamkubali jambo Hilo. Maana, unajua, huwezi kuficha jambo hilo sasa hivi. Huwezi.

Lakini hebu niwaonyeshe tu jambo fulani. Kama Mathayo 28:19 ilisema, "Basi enendeni, mkayafundishe mataifa yote, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu," nao wakageuka, na kila mtu ambaye aliwahi kubatizwa alibatizwa kinyume chake, wakabatiza katika Jina Lake

Yesu Kristo, kwani hata katika wakati wote wa Biblia na kwa miaka mia tatu baada ya wakati wa Biblia, mpaka lile Baraza la Nikea. Ndipo wakachukua mafundisho ya sharti badala yake. Kuna tofauti gani, kama halijafunuliwa?

90 Na je! Mnajua Kitabu chote, Biblia nzima, ni ufunuo? Hivyo ndivyo inavyokupasa kujua ukweli kati ya huu na mwingine, ni kwa sababu ni ufunuo. Na ufunuo lazima upatane kabisa na Neno, sio kinyume cha Neno. Unasema, "Vema, mimi, lilifunuliwa kwangu." Basi kama ni kinyume cha Neno, kamwe halikutoka kwa Mungu. Hiyo ni kweli.

Sasa kama unataka kuchukua Mat- … Mathayo 16:18. Yesu alisema, Yeye Mwenyewe, ya kwamba Kanisa lote, Kanisa Lake, lingejengwa juu ya ufunuo Wake wa kiroho, ambao ni Neno. "Nakwambia ya kwamba wewe ndiwe Petro … Na mwili na damu kamwe havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili. Na juu ya mwamba huu …"

Sasa, najua, marafiki zetu Wakatoliki pale, mnasema, "Lilijengwa juu ya Petro, na Petro mtume, kwa hiyo, *Fulani*, katika makubaliano ya kimitume, uhalifa."

Waprotestanti walisema, "Lilijengwa juu ya Yesu Kristo."

Si kuwa tofauti, bali chukua tu yale aliyosema! Yeye alisema, "Mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili. Na juu ya mwamba huu"(ufunuo wa kiroho wa kile Neno ni nini)"Nitalijenga Kanisa Langu; wala malango ya kuzimu hayatalitikisa." Mkewe hatajaribiwa na wanaume wengine. "Nitalijenga Kanisa Langu, wala milango ya kuzimu kamwe haiwezi kulitikisa."

91 Na Habili na Kaini, katika bustani ya Edeni. Kaini alitoa mawazo yake mwenyewe, akasema, "Sasa, angalia, Mungu ni Mungu mwema. Yeye yuko juu ya maumbile yote, kwa hiyo nitachukua maharagwe na viazi, na nitachukua ma—maua, nami nitamfanyia madhabahu ya kupendeza sana." Hilo ni kanisa. Akapiga magoti. Alimwamini Mungu. Alimwabudu Mungu, akainua mikono yake, na kutoa sadaka hii. Yeye alifanya kila kitu cha kidini ambacho Habili alifanya.

Habili alijenga madhabahu ya namna ile ile. Lakini wakati Habili alipoleta yake, alimleta mwana-kondoo. Sasa, Kaini alifikiria kwamba, alipokuwa akifanya kinga kwa ajili ya dhambi, kwamba baba yake na mama yake lazima walikula tunda, kama walivyofundishwa katika bustani ile. Lakini Habili, kwa ufunuo wa Kiungu, alijua ya kwamba damu ndiyo iliyofanya jambo hilo. Kwa ufunuo wa Kiungu! Na Biblia ilisema katika Waebrania, sura ya 12, sura ya 11, kwamba, "Habili, kwa imani, (ufunuo), alimtolea Mungu sadaka iliyo bora kuliko ya Kaini, ambayo kwayo Mungu alishuhudia kwamba yeye alikuwa mwenye haki." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Amina! Ndugu, dada, ni dhahiri tu kama cho chote kiwezacho kuwa, kwangu. Hilo hapo jambo lote.

92 Sasa juu ya *Ndoa Na Talaka*, mnaona, haina budi kufunuliwa. Mpaka itakapofunuliwa, huijui. Lakini Yeye aliahidi katika siku hizi za mwisho, katika wakati huu, ya kwamba kila siri iliyofichwa katika Biblia ingefunuliwa. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Ufunuo, mlango wa 10! Yesu aliahidi jambo hilo, ya kwamba siri hizi zote zilizofichwa juu ya—juu ya Ndoa na Talaka, siri hizi zingine zote zilizofichwa, zingefunuliwa katika wakati wa mwisho. Sasa mnakumbuka, ile Sauti ilisema, "Nenda Tucson." Kumbukeni ile Nuru ya kisiri angani; yule Malaika wa saba amesimama pale; kurudi, na kule kufunguliwa kwa ile Mihuri Saba? Angalia kilichotukia. Hiyo ni kweli.

Sasa mbele kidogo tu. Lakini sasa, sikilizeni! Najua wakati wenu wa kwenda kula umekaribia, bali ninakula tu vizuri. [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

93 Angalia, sasa, mwanamke ana mahali pake, naye ni kito cha thamani. Sulemani, mtu huyu aliyekuwa na wake elfu kumi…au alikuwa na wake elfu, hasa, alisema kwamba, "Mwanamume aliyempata mke, amepata kitu chema." Alisema, "Mwanamke mwema ni kito katika taji yake," yaani heshima. "Lakini asiye na haki ni maji katika damu yake," yaani maisha yake. Yeye alisema, "Kwawezekana kupatikane mwanamume mmoja mwenye haki katika elfu moja," Sulemani alisema hivi, "lakini," akasema, "usingempata mwanamke mmoja mwenye haki katika elfu moja." Sulemani alisema hivyo, mnaona. Sasa angalia jambo hilo, ndivyo ilivyo.

Lakini, unaona, ewe mwanamke, wewe u—wewe ni kito kama unataka kuwa kito, lakini tamaa yabidi itokane na wewe. Na unaona kwa nini *Ndoa Na Talaka* ilikuwepo, na Yesu alielekeza nyuma huko, ilikuwa kwa sababu wa aina yenu ndiye alikuwa chanzo cha dhambi yote. Hiyo ndiyo sababu ndoa za wake wengi na talaka, na kadhalika, zilianzishwa. Hapo mwanzo halikuwa hivyo, wala haitakuwa hivyo ulimwenguni kote.

94 Mwangalie Yakobo, ambaye kwake walitoka wale wazee. Alikuwa na angalau wanawake kumi na wawili. Alioa dada wawili, na pia alikuwa na masuria, wanawake wa kukaa nao kimila alioishi nao. Na hao wazee bila shaka walizaliwa na hao masuria. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Unaona, yakubidi kulifanya Neno lifuatane kikamilifu.

Loo, nina kurasa juu yake. Kama kasisi akihoji juu yake, nasi tupate kukutana pamoja, tungeweza kulizungumzia. Lakini hakika, kama ana hali yo yote ya kiroho, anaweza kuona papa hapa ni Kweli. Hakuna swali Kwake.

Mwanamke mzuri ni kitu kizuri. Ninajua jambo hilo. Ninajua hivyo kwa wanawake halisi. Nimekutana na wanawake halisi ambao ni wa kweli, halisi tu kama mwanamume yeyote aliyewahi kutembea.

Yeye ni kiumbe kilichotolea kwa kingine na ni kipande chake, na katika kule kuanguka mwanamume alimsikiliza yeye. Yeye alininii tu … Yeye ni sehemu yake. Lakini, ni juu yake, yeye ameumbwa ili aweze kuwa mchafu, naye anapewa haki ya kukataa au kukubali. Hilo ni kinyume cha maumbile asili hapo mwanzo, unaona, bali hivyo ndivyo ilivyo.

95 Sasa ni saa sita, kwa hiyo nitaacha tu kitu fulani hapa kwa dakika chache. Ninataka kuwaulizeni jambo fulani.

Sasa, kumbukeni, ninasema jambo hili kwa kundi langu tu. Na huko nje hewani, ninasema jambo hili kwa wafuasi wangu tu. Ujumbe huu ni wao tu, na yale nitakayosema hapa.

Mhudumu ye yote, yeye, hao ni wake, ndiyo, yeye ni mchungaji wa kundi, acha atende cho chote anachotaka. Hiyo ni juu yake na Mungu. Kasisi ye yote, mhubiri yeyote, hiyo ni juu yako, ndugu yangu.

Ninazungumza tu hapa Jeffersonville, mahali pekee ambapo ningezungumzia jambo hili, ni kwa sababu ni kundi langu mwenyewe. Ndilo kundi ambalo Roho Mtakatifu amenipa kulifahamu na kuwa msimamizi wake, ataniwajibisha kwa ajili yake. Na watu wangu hawa wamekuwa waongofu hapa kutoka kote nchini, ambao nimewaongoza kwa Kristo. Na, watoto wadogo, niko hapa kuwasaidia, nami ni rafiki yenu. Huenda mkafikiri ninasema dhidi yenu; Ninasema jambo hili, mnaona, kwa manufaa yenu. Ninawapenda. Na kama sivyo ilivyo, Mungu ndiye Hakimu wangu. Unajua ninawapenda.

96 Hili ni jambo zito mno, sikujua jinsi ya kulieleza. Nitafanya nini, na huku nina wanaume na wanawake wanaoketi kwenye kusanyiko langu, baadhi yao wameolewa na kuoa mara mbili au mara tatu? Wanaume wazuri na wanawake wazuri, wote wamechanganyikiwa! Ni kitu gani kilichofanya jambo hilo? Mafundisho ya uongo, bila shaka, bila ya kumngojea Bwana.

"Aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe." Sio aliowaunganisha mwanadamu; aliowaunganisha "Mungu"! Unapopata ufunuo wa moja kwa moja kutoka kwa Mungu, huyo ni mkeo, na jambo lile lile, huyo ni wako maishani mwako mwote. Mnaona? Lakini aliowaunganisha mwanadamu, mtu ye yote anaweza kuwatenganisha. Lakini aliowaunganisha Mungu, mwanadamu ye yote asithubutu kuwagusa. "Kila anaowaunganisha Mungu," Yeye alisema, "mwanadamu asiwatenganishe." Sio wale waliounganishwa na hakimu fulani aliyelewa nusu au na kitu kingine, au mchungaji fulani aliyerudi nyuma akiwa na tita la kanuni za imani katika kitabu, ambaye angewaruhusu kufanya kitu cho chote ulimwenguni, na Neno la Mungu likiwa limekaa pale pale. Mnaona? Ninazungumza juu ya kile Mungu alichounganisha pamoja.

97 Sasa nitawaambia jambo hili. Mimi ni mwangalifu sana kwa yale ninayowaambia. Sitaki kuwa mkali kwenu enyi watu. Sitaki kuwa mkali kwenu, ndugu zangu wachungaji. Simaanishi jambo hilo. Lakini ninawajibika, nikitambua ya kwamba jambo hili limewekwa mikononi mwangu. Na kama … Siwezi kulishikilia. Na sijui jinsi ya kulitoa, na najua kanda hii italitoa. Loo, jamani, nitajitayarisha, ofisi iko wazi, sababu hili hapa linakuja. Mnaona?

Kama tu ilivyokuwa kwenye *Uzao wa Nyoka*, lakini imethibitishwa kabisa kuwa ni kweli. Nina makaratasi papa hapa, kutoka kwenye gazeti, ambapo wanawake sasa hivi … na hata katika—katika ninii kuu … Baadhi ya majimbo makuu ya askofu yana picha za asili, nyoka akitambaa kwenye mguuu wa mwanamke, na jinsi tu anavyojizungushia kwake; yeye hupata kila namna ya nyege na kadhalika, kitu ambacho mwanamume asingeweza kumgusa nacho kamwe, huku huyu nyoka mkubwa amejizungushia mwilini mwake, na kadhalika. Hiyo ni kweli kabisa. Na inazidi kuwa mbaya zaidi, na itakuwa mbaya zaidi. Nyoka, hakuwa nyoka, ... asingeweza kujuana kimwili naye wakati alipokuwa nyoka, lakini kumbuka…

98 Nilikuwa na mjadala hivi majuzi na … sio mjadala, mhudumu tu wa Assembly of God na mwenzangu, akasema, "Umekosea, kwenye jambo Hilo."

Nikasema, "Vema, huenda nikawa nimekosea. Ningetaka wewe uniambie."

Yeye alisema basi, akaendelea na kuanza kuzungumza juu ya jambo hilo. Jambo la kwanza mnajua, yeye mwenyewe alipotea. Na jambo moja alisema, alisema, "Ndugu Branham, kiko wapi cha jinsi hiyo? Mungu alisema 'moja kwa jinsi yake.' Sasa ki wapi kiumbe hicho ulichosema kiko kati ya mwanadamu na mnyama, ambacho sayansi haiwezi kukipata sasa? Kiko wapi?" Kasema, "Je! Kipo duniani? Kilikuwa sokwe mtu?"

"La, kwa sababu damu ya sokwe haitachanganyikana na mwanamke, hakuna mnyama mwingine

atakayechanganyikana naye. Hapana, haitachanganyikana, wala shahawa ya mwanamume haitachanganyikana na—na ya kike. Haiwezekani." Haitafanya hivyo."

"Basi yuko wapi huyo mnyama mwenyewe? Sasa, Mungu alisema, 'Kila kitu kizae kwa jinsi yake.'"

Nilingojea kwa dakika moja tu. Na utamu wa Roho Mtakatifu ukasema, "Mwambie, 'Kiko hapa.'"

Sasa, mwanzoni nilisema, "Vema, huenda ikawa kimetoweka."

Akasema, "Lakini, Ndugu Branham, hilo, tunazungumza kuhusu Neno, sivyo?"

Nikasema, "Naam, bwana." Nami nikasema, "Wao, bila shaka, wanadai ya kwamba vitu hivyo vingine, kama dinosa na—na mamothi, na kadhalika, mamothi, mamothi, ndio namaanisha, hawapo tena, na kadhalika." Nikasema, "Ingewezekana kuwa hivyo."

Yeye alisema, "Ndugu Branham, tunazungumzia juu ya uthibitisho wa Neno. Kama dhambi iko hapa; basi, ile dhambi ya asili, inapaswa kuwepo papa hapa pia."

Nami nikasema, "Bwana Yesu, Wewe ulisema, 'Msifikirifikiri mtakalosema mnapokuja mbele za watu, kwa sababu mtapewa hilo katika saa ile.' Bwana, niseme nini?" Akasema, "Mwambie, 'Kipo hapa.'" Ni kama tu ninavyoona maono jukwaani.

Nikasema, "Kiko hapa," bila kujua ni wapi.

Akasema, "Wapi?"

Na kabla hata sijawazia, Yeye alisema, "Ni nyoka."

99 Hivyo ndivyo ilivyokuwa hasa, kwa kuwa yeye si mnyama tena. Alilaaniwa na akafanywa aende kwa tumbo lake maishani mwake mwote. Yeye yuko hapa. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Na bado katika kitendo hicho ambacho alitenda, bado kuna dhambi ile ile inayotenda kazi kwa mwanamke, kama kujuana kimwili na mwanamume hivyo. Hapo ndipo mwanamke anapokuwa na macho meupe na kadhalika, wakati nyege zake zinapozidi kwa mbali mno yale mwanamume ye yote angeweza kutenda.

Nitakoma hapo maana tuko katika umati uliochanganyikana. Nitawapata watu fulani, nita- … tutazungumza zaidi juu ya jambo hilo. Nina makaratasi yote na kadhalika papa hapa, papa hapa kwenye mkono wangu wa kuume sasa hivi, nami nilitaka kuwaleteeni asubuhi hii. Nilikuwa nichukue siku nzima juu ya jambo hili, lakini nitafunga sasa kwa kusema hivi.

100 Hili ni kwa kanisa langu tu. Si kanisa langu … Kundi dogo linaloniamini na kunifuata, hili ni kwa ajili yao.

Juzijuzi, nikijua kwamba ninapowaambia kitu cho chote, lazima kije BWANA ASEMA HIVI, basi nilikuwa na Maandiko kama Yeye alivyonifunulia. Lakini, "Bwana Mungu, naweza kuliambia kusanyiko hilo nini? Nitasababisha watu kuachana. Wanaume watakuwa wameketi sebuleni na nje uwanjani, na kila mahali penginepo, 'Nimwache?' Wanawake, 'Nimwache mume wangu?' 'Nifanye nini?'" Nikasema, "Bwana, nifanye nini?"

Kitu fulani kiliniambia, "Nenda kule mlimani, nami nitazungumza nawe."

Na wakati nilipokuwa kule juu mlimani, bila kujua ya kwamba kule chini Tucson walikuwa wanaiona hiyo. Lakini hata waalimu waliwaita watoto toka…msichana wangu mdogo na wengineo, toka darasani, kasema, "Angalieni kule mlimani! Kuna Wingu la moto lenye sura ya kaharabu linapaa angani na kushuka chini, linapaa juu angani na kushuka chini."

101 Bibi Evans, uko hapa? Ronnie, wewe uko hapa? Nikashuka nikarudi kwenye kile kituo, huyu mvulana kwenye kituo cha mafuta, kituo cha mafuta cha Evans pale. Na kabla sijajua ambacho yule mvulana anataka kusema, alinishangaza, akasema, "Ndugu Branaham, ulikuwa kule mlimani, sivyo?"

Nikasema, "Unamaanisha nini, Ronnie? La," unaona, kuona atafanya nini. Mara nyingi vitu hutukia, mimi siwambii, huwaambii watu. Ikawa … Jambo ni kwamba, unaona mengi sana yakitukia, inakuwa ni jambo la kawaida kwako. Mnaona? Siwaambii tu watu. Nikasema, "Ronnie, ulikuwa nini …"

Akasema, "Ninaweza kukuonyesha mahali ulipokuwa." Kasema, "Nilimwita mama, nasi tukasimama hapa na kuangalia Wingu hilo likining'inia kule juu, likipanda juu na kushuka. Nikasema, 'Haina budi kuwa ni Ndugu Branham anayeketi kule juu mahali fulani. Huyo ni Mungu akinena naye.'"

Na mji mzima, watu, waliliangalia. Katika siku yenye kung'aa bila mawingu mahali po pote hata kidogo, huku Wingu hili kubwa la kaharabu likining'inia pale; likishuka chini kama mfereji, na kurudi na kuenea.

102 Enyi marafiki, halafu ninafunga, mnaweza kutoka kwenye hili. Hapo ndipo wakati Nilipokuwa nikifunuliwa hili, yale nitakayowaambia sasa hivi, kwa hiyo msilikose.

Sasa ninazungumza na wafuasi wetu tu, ambao wananifuata mimi na Ujumbe huu tu, si walio nje. Nishuhudieni jambo hili mbele za Mungu. Ni kwa kundi hili tu!

Sasa tunakutwa katika mchafuko huu kwa sababu ya theolojia iliyofafanuliwa vibaya. Hiyo ni kweli? Hiyo ndiyo sababu ninyi wanawake mmeolewa mara ya pili, nanyi wanaume, kwa sababu ya theolojia iliyofafanuliwa vibaya. Sasa nataka kuwaonyesha jambo fulani ambalo Yeye aliniambia.

Na kama Mungu, Muumba wetu, aliulizwa hilo swali alipokuwepo hapa duniani, Yesu Kristo; na wakati nabii wake wa kukomboa alipokuja, Musa, huko chini Misri, kuwatoa wale wana kutoka—kutoka Misri, kuwaweka kwenye nchi ya ahadi; na Yesu alisema hapa kwamba Musa aliwaona watu katika hali hii, naye akawapa hati ya talaka, kwa sababu hali ilikuwa vile alivyokuwa. Musa aliyakuta hayo, kama, "Na amwache…" Mungu alimruhusu Musa, Yule nabii aliyetumwa kwa hao watu, kuwapa hii hati ya talaka.

103 Na katika Wakorintho wa Kwanza, m—mlango wa 7, kifungu cha 12 na 15, katika nabii wa Agano Jipya, Paulo, ambaye alikutana na jambo lile lile kanisani, na kunena jambo hili, "Huyu ni Mimi, si Bwana." Hiyo ni kweli? Kwa sababu ya hali za talaka.

"Haikuwa hivyo tangu mwanzo." Lakini Musa aliruhusia, naye Mungu akalitambua kuwa ni haki. Na Paulo pia alikuwa na haki, wakati alipolipata kanisa lake katika hali hiyo.

Sasa mnaamini Hili kuwa ni kweli, na mnaamini linatoka kwa Mungu! Na kwa udhihirisho wa Wingu Lake na Ujumbe Wake ambao umenifikisha umbali huu, je, Mungu huko mlimani asingeniruhusu mimi kutenda jambo lile lile, kuwaruhusu ninyi mwendelee jinsi mlivyo, na msitende jambo hilo tena! Nendeni na wake zenu mkaishi kwa amani, kwa maana wakati umechelewa. Kuja kwa Bwana kumekaribia. Hatuna wakati wa kuvunja mambo haya. Usithubutu kujaribu kufanya jambo hilo tena! Ninazungumza na kusanyiko langu tu. Lakini kama umeoa … Na Mungu alinishuhudia kuhusu jambo hilo, kule mlimani, kwamba ningeweza kunena jambo Hili, ufunuo wa kiroho, kwa sababu ya kule kufunguliwa kwa zile Muhuri Saba, na hili ni swali katika Neno la Mungu. "Waacheni waendelee jinsi walivyo, wasitende dhambi tena!"

104 "Haikuwa hivyo tangu mwanzo." Hiyo ni kweli, haikuwa hivyo, na haitakuwa mwishoni. Lakini katika hali za kisasa, kama mtumishi wa Mungu … Sitajiita mwenyewe nabii Wake; lakini ninaamini pengine, kama nisingepelekwa kwa ajili ya jambo hilo, ninaweka msingi kwa ajili yake huyo ajapo. Kwa hiyo chini ya hali za kisasa, ninakuamuru uende nyumbani kwako, pamoja na mke wako sasa. Kama una furaha naye, ishi naye, walele watoto wako katika maonyo ya Mungu. Lakini Mungu na akurehemu kama ukifanya hivyo tena! Wafundisheni watoto wenu wasije wakafanya jambo kama hilo, waleeni katika maonyo ya Mungu. Na sasa kwa kuwa mko jinsi mlivyo, hebu twendeni sasa, katika majira ya jioni yaliyochelewa ambamo tunaishi, na "tukaze mwendo tuifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu katika Kristo," ambapo mambo yote yatawezekana.

Mpaka nitakapowaona usiku wa leo, Bwana Mungu awabariki, tunapoomba.

105 Bwana Mungu, tunakushukuru. Tunakupa sifa. Wewe ni Yehova yule yule mkuu uliyemruhusu Musa. Musa, yule mtumishi, naye angewaambia nini watu wake? Na, Mungu, ulimruhusu kutoa hati ya talaka. Paulo, yule mtume mkuu aliyekuwa mwandishi wa Agano Jipya, kama vile Musa alivyokuwa wa lile la Kale. Musa aliandika Torati na wakati ya torati. Wengi wa manabii, maneno yao yaliingizwa ndani Yake, bali Musa aliandika zile Torati. Nawe ukamruhusu kuandika, kuwaandikia hati ya talaka, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao.

Yule Mtakatifu mkuu aitwaye Paulo, akiwa mwandishi wa Agano Jipya, aliweza pia kutoa tamshi kama hilo, kwamba, "Ninazungumza katika hali hizi; mimi, sio Bwana."

106 Ndivyo ilivyo leo, Bwana Mungu, katika mwisho wa ulimwengu, kwa kuwa tuko hapa chini ya rehema ya Mungu, tukijua ya kwamba karibuni tutajibu Mbele Zake. Na kwa kuwa Wewe umefanya mengi sana, Bwana, nina hakika, machoni pa watu hawa, watashikilia Hili kama linalotoka Kwako. Na kushuhudia hapa leo, wakiwepo watu wengi wanaoketi hapa ambao hata waliona Ishara ile juu kule mlimani, ambako Malaika wa Bwana walikuja katika upepo wa kisulisuli, ambao ulikuja katika wale Malaika saba, ambapo ufunuo wa Siri zile Saba ulifunuliwa, na Malaika yule yule, katika upande ule ule, kwenye mlima ule ule, siku ambayo Hili lilifunuliwa.

Mungu, ninaomba ya kwamba watu wataenda nyumbani wakishukuru kwamba Mungu amewapa neema hii. Nililinena tu, Bwana, kwa ruhusa. Nami ninasema tu jambo hilo kwa ruhusa, Bwana. Na wajalie watu wawe na shukurani sana hivi kwamba hawatajaribu kamwe kutenda dhambi hiyo tena! Na jalia wasijaribu kamwe kutenda dhambi yo yote, bali wakupende Wewe kwa mioyo yao yote. Bwana, zifanye familia hizi ziwe na furaha, na jalia zikue na kuwalea watoto wao katika maonyo ya Mungu.

107 Kwa kuwa, Ujumbe wangu uliokuwa moyoni mwangu umetolewa, Bwana. Nimefanya yote nijuayo jinsi

ya kufanya. Na Shetani amenipiga vita kwa majuma kadha, na masaa mengi bila usingizi. Lakini sasa naliamuru Hilo, Bwana, kwa watu hawa, kwamba wajifunze Hilo, na waende na kukuishia Wewe. Lijalie, Bwana. Limeondoka mabegani mwangu sasa. Wako mikononi Mwako. Naomba kwamba Wewe utawabariki.

Bariki leso hizi, Bwana, ambazo zimewekwa hapa hivi punde, kwa ajili ya wagonjwa na wanaoteseka. Jalia usiku huu uwe mmoja wa zile kuu sana, zenye nguvu, ambapo watu wote wataponywa. Tujalie, Bwana. Tubariki sote pamoja.

108 Tujalie twende kwa amani, wenye furaha na wanaoshangilia, kwa sababu Mungu wa uumbaji ametuonyesha "tangu mwanzo," Naye ametukirimia, na machafuko yetu tuliyo nayo, neema Yake tena, katika siku hii ya mwisho. Ee Mungu Mkuu na wa Milele, jinsi tunavyokushukuru kwa jambo hilo! Na jalia mioyo yetu iwe na furaha sana, hata hatutakuwa na shauku nyingine ya kukutendea dhambi. Katika Jina la Yesu. Amina.

Nampenda, (kwa nini usimpende?) Nampenda
Kwa sababu Yeye alinipenda
Na kununua wokovu wangu
Kalvari …

Ninalisema sasa ili wahudumu wafahamu. Hii ni kwa wale wanaofuata Ujumbe huu tu!

Loo, mna furaha? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Nimewaambieni Kweli, BWANA ASEMA HIVI, kote kote! ["Amina!"]

Sasa hebu na tusimame na kuinua mikono yetu, tunapoimba tena, "Nampenda." Ninampenda kwa neema Yake. Ninampenda kwa rehema Yake. Ninampenda kwa ajili ya Neno Lake. "Na Neno la Bwana liliwajia manabii!"

Nampenda.

Njoo, ndugu. [Ndugu Branham anamwita mtu fulani aje aruhusu kusanyiko litawanyike—Mh.]

MESSAGE hub online
www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7